**Sera** yaja diaspora kununua nyumba, wateja wa Morocco Square wakabidhiwa
UKURASA 4



**Ukifanya** haya mama mkwe atakufurahia
UKURASA 11


MAISHA
Nipashe Jumapili
Baba, Mama na Mwana
Jilambe na sambusa za nyama
UREMBO: Fahamu haya kuhusu rangi ya jeli
KATUNI
Nani kakwambia mpaka uagize gauni la harusi
UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 2, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581359

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# ‘Siogopi kitanzi’



**MSHTAKIWA** atoa kauli za kushtusha kortini. Hakimu amwambia ...
*Endelea ukurasa. 3*

UKURASA WA 2

## BEI ELEKEZI MBOLEA NCHINI ZATANGAZWA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetangaza bei elekezi za mbolea kwa wafanyabiashara zitakazotumika kwa siku 46 kuanzia jana.
Kwa mujibu wa tangazo lao...





UKURASA WA 17

## KAMATI UTARATIBU MPYA MIKOPO MAKUNDI MAALUM YAKABIDHI RIPOTI

KAMATI maalum iliyoundwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuangalia utaratibu mzuri unaoweza kutumiwa na serikali kutoa mikopo kwa makundi maalum maarufu asilimia 10, imekamilisha kazi...



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akiwapa samaki chakula katika moja ya bwawa la kufugia samaki lililobuniwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), baada ya kufungua wiki ya maadhimisho ya miaka 60 ya JKT katika viwanja vya Suma JKT House, Medeli Mashariki, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

## Makamu wa Rais aagiza mafunzo JKT yajikite katika ujuzi kiteknolojia

UKURASA 2

# Bodaboda yakatisha uhai wa mbunge



**Ni** aliyeibua ukatili wa askari-pori kwa wananchi hivi karibuni... *Endelea Uk. 2*

**MICHEZO** **SIMBA YAANZA MAZUNGUMZO NA KOAUME** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Wagombea na wananchi wa kata ya Magubike, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro wakitazama fomu za uteuzi za wagombea walioteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kubandikwa katika eneo la wazi jana, ili kutoa fursa ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea asiyekuwa na sifa. **PICHA: MROKI MROKI WA NEC**

# Bodaboda yakata uhai wa mbunge

**Na Nebart Msokwa,**
MBARALI

MBUNGE wa Mbarali mkoani Mbeya, Francis Mtega (CCM), amefariki dunia baada ya pikipiki aliyokuwa anaendesha kwenda shambani kugongwa na trekta (Power Tiller).

Taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Kanali mstaafu Denis Mwila, ilibainisha kuwa mbunge huyo alipata ajali hiyo jana alasiri katika eneo la Kibaoni, Kata ya Ihahi, barabara ya Chimala-Kapunga.

Kanali Mwila alisema trekta lililomgonga mbunge huyo lilikuwa linaendeshwa na kijana Alex Kibega (18), mkazi wa Kibaoni. Chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa trekta hilo ambaye alikuwa anaendesha bila tahadhari yoyote.

"Kijana huyo aliyekuwa anaendesha trekta hilo amekamatwa na anaendelea kushikiliwa. Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali kwa ajili ya taratibu zingine," alisema Kanali Mwila. Alisema kuwa baada ya ajali hiyo, mbunge huyo alikimbizwa katika Hospitali ya Misheni Chimala kwa ajili ya matibabu kabla ya kuthibitishwa kuwa alikuwa tayari ameshafariki dunia.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Misheni Chimala, Dk. Peter Kigombola, alithibitisha kupokea mwili wa marehemu. Walipomfanyia uchunguzi wa awali, walibaini kuwa alikuwa tayari ameshafariki dunia.

Alisema walipata taarifa kuwa mbunge huyo amepata ajali na hivyo wakaandaa timu ya madaktari kwa ajili ya kuokoa maisha yake lakini walipobaini alikuwa ameshafariki dunia, walihifadhi mwili wake na kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali.

"Tulipouchunguza mwili huo, tumebaini kuwa alikuwa na majeraha kichwani, mgongoni na tumboni, lakini inasemekana kwamba baada ya kugongwa lile trekta lilimpitia tena mgongoni," alisema Dk. Kigombola.

Alisema kuwa baada ya kutoa taarifa serikalini na kwa viongozi wa chama, waliagiza mwili huo uhamishwe na hivyo wakauhamishia katika Hospitali ya Wilaya kwa ajili ya kuhifadhiwa. Ofisi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa cha Bunge - Dodoma, pia ilithibitisha kutokea kwa kifo cha mbunge huyo.

Alisema Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na familia ya marehemu inaratibu mipango ya mazishi na taarifa zaidi zitaendelea kutolewa.

Viongozi mbalimbali wa serikali na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, jana walituma salamu za pole kwa familia ya marehemu na wananchi wa Jimbo la Mbarali kufuatia tukio hilo.

Mwezi uliopita, mbunge huyo alikuwa miongoni mwa wawakilishi wa wananchi walioibua hoja 'nzito' bungeni, alipowasilisha jambo la dharura kuhusu alichokiita ukatili wa askari-pori wa Hifadhi ya Taifa Ruaha dhidi ya wakazi wa Mbarali.

Kutokana na hoja hiyo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliagiza timu ya mawaziri watatu iende Mbarali kufuatilia suala hilo, huku akiwataka wampatie majibu siku iliyofuata. Hatua zilichukuliwa.

# Mpango aagiza mafunzo JKT kujikita katika teknolojia

**Na Renatha Msungu**,
DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameliagiza Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuwekeza zaidi katika matumizi ya teknolojia katika kuwafundisha vijana kwa kuwa hivi sasa dunia inakwenda na wakati bila kutumia msuli.

Aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akizindua Wiki ya Maonyesho ya JKT inayokwenda sambamba na uzinduzi wa mnara wa maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo tangu kuanzishwa kwake.

Dk. Mpango alisema jeshi hilo linapaswa kutambua utaalamu walionao vijana hao na kuuendeleza ili kuwazalisha watakaoliletea taifa tija, pia familia zao.

"Ninatoa msisitizo katika suala la matumizi ya teknolojia.

Ninaomba JKT mlifanyie kazi suala hilo ili kuhakikisha vijana wanatoka na utaalamu wa kutosha utakaowasaidia," alisema.

Mbali na hilo, Makamu wa Rais pia aliitaka jeshi hilo kuweka mikakati ya kuwa na ghala la chakula kwa ukanda wa Afrika kwa sababu uwezo huo wanao kutokana na jitihada wanazofanya katika kilimo.

Dk. Mpango pia aliitaka jeshi hilo kuzalisha kwa wingi chakula cha samaki ili kukidhi mahitaji ya wale wanaokabiliwa na uhaba ikiwa ni pamoja na kushawishi jamii kujikita katika ufugaji wa mazao hayo.

Alisema JKT wanapaswa kutoa elimu kuhusiana na kilimo wanachofanya ikiwamo kuwa sehemu ya shamba darasa kwa watanzania ili kuzidi kuchagiza uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini.

"Ninajua hili linawezekana kabisa kwa JKT, uwezo mnao na wataalamu wa kilimo mnao pia kwa ajili ya kuelekeza namna ya kilimo kinavyofanywa," alisema Dk. Mpango.

Alisisitiza jeshi hilo kuunga mkono jitihada za serikali katika utunzaji wa mazingira, akitaka kambi zote katika jeshi hilo ziweke mikakati ya kudhibiti taka za plastiki ambazo zinachangia uchafuzi wa mazingira.

Dk. Mpango pia alisema changamoto zote ambazo jeshi hilo limeziwasilisha, atazifikisha kunakostahili ili zifanyiwe kazi.

Makamu wa Rais pia aliliagiza jeshi hilo kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kupanda miti ya mbao ili kusaidia kutengeneza bidhaa bora kwa kutumia rasilimali za nchini.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, alisema jeshi hilo liko tayari kutekeleza yote yalioagizwa huku akitoa pongezi kwa JKT kutokana na maandalizi mazuri ya maonyesho hayo.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alisema katika wiki ya maonyesho, kutakuwa na mambo mbalimbali ambayo yatafanywa na JKT kupitia vikosi vyake mbalimbali na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi.

# Bei elekezi mbolea nchini zatangazwa

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetangaza bei elekezi za mbolea kwa wafanyabiashara zitakazotumika kwa siku 46 kuanzia jana.

Kwa mujibu wa tangazo lao lililotolewa jana na kutiwa saini na Mkurugenzi Mtendaji wa NFRA, Dk. Stephan Ngailo, mbolea zinatakiwa kuuzwa kwa bei elekezi au chini yake.

Kupitia tangazo hilo, kiongozi huyo alisema bei hizo elekezi za mbolea zitaanza kutumika kuanzia Julai Mosi hadi Agosti 15 mwaka huu.

"Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 4 (1) (u) cha Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009 na Kanuni ya 56 ya Kanuni za Mbolea za Mwaka 2011 kama zilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2017.

"Katika kutekeleza majukumu yake, NFRA imefanya mapitio ya bei elekezi kwa mbolea aina tisa; tano zinazoingizwa kutoka nje (DAP, AREA, CAN, SA na NPKs) na nne zinazozalishwa na viwanda vya mbolea vya Itracom (Fomi Otesha na Fomi Kuzia) na Minjingu (Nafaka Plus na Top Dressing)," inasomeka sehemu ya tangazo hilo.

Pia alisema bei za mbolea zinazoagizwa nje ya nchi zimezingatia gharama za ununuzi, usafirishaji uingizaji, ufungashaji, usambazaji na faida ya mfanyabiashara na zile zinazozalishwa nchini nazo zimezingatia gharama za upatikanaji wa malighafi, uzalishaji, vifungashio, kufungasha, usimamizi na faida ya uzalishaji na muuzaji wa rejareja kusambaza hadi kumfikia mkulima.

"Serikali imeelekeza aina moja ya mbolea kuuzwa kwa bei inayofanana kwa wakulima kote nchini. Hakuna mfanyabiashara atakayeruhusiwa kuuza mbolea nje ya mpango wa ruzuku.

"Hivyo, tofauti kati ya bei elekezi kwa kila eneo na bei ya mkulima italipwa na serikali kama ruzuku kwa mkulima kwa lengo la kumpunguzia makali ya bei. Vifungashio vya ujazo wa kilo tano vitauzwa kwa bei elekezi sokoni," alisema.

Ngailo alisema pamoja na kwamba mpango wa ruzuku ya mbolea unalenga kuwapunguzia makali ya bei wakulima, wafanyabiashara wachache wasio waaminifu wanaweza kutumia fursa hiyo kuwalaghai na kununua kwa majina na baada ya hapo kuitorosha kwenda nchi jirani. "Hali hii itahatarisha utoshelevu wa mbolea kwa wakulima na pia kuingizia hasara serikali katika fedha zinazotoa kama ruzuku kwa lengo la kumnufaisha mkulima na kuongeza uzalishaji nchini," alisema.

Aliongeza kuwa pamoja na elimu ambayo serikali inaendelea kutoa, ni vyema mamlaka zote zikashirikiana na wadau hususani katika mikoa ya mipakani kama Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Kagera, Kilimanjaro na Arusha kuhakikisha haitoroshwi kwenda nchi jirani.

"Ninatoa onyo kali kwa wafanyabiashara wachache wenye tabia hizo au mpango wa kutorosha mbolea ya ruzuku kutothubutu kufanya hivyo kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Endapo kutakuwa na haja ya wafanyabiashara kuuza nje ya nchi, basi wafanye hivyo kwa kuzingatia taratibu na sheria na siyo kutorosha," alionya.



Baadhi ya Wananchi wakiwa wamevalia vifaa maalumu vya uhalisia pepe vinavyoonyesha maendeleo ya mradi wa bwawa la kufua umeme wa maji la Julius Nyerere (JNHPP), walipotembelea banda la Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), katika maonyesho ya 47 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam jana. **PICHA: MAULID MMBAGA**

KESI MAGUNIA YA MKAA

# Anayeshtakiwa kumuua mke wake adai haogopi kunyongwa

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, amedai haogopi kunyongwa hadi kufa wala adhabu nyingine yoyote.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo amedai kuwa anataka "anyongwe kwa haki" kwamba aliua bila kukusudia.

Katika kesi hiyo ya mauaji Na. 4 ya mwaka 2019, mshitakiwa Luwonga ambaye ni mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kuwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

Luwonga alidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemalira wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam baada ya kusomewa maelezo ya mashihidi 28 na vielelezo 14 na upande wa mashitaka.

"Kitu ambacho ninakikataa mheshimiwa hakimu, ni kuwa niliua kwa makusudi. Mimi sikuua kwa makusudi. Hata ninyongwe leo hadi kufa kwa kile cha kweli, nitaangamia kimwili lakini siyo kiroho.

"Siogopi kunyongwa wala siogopi adhabu yoyote ile, lakini ninataka kama nikinyongwa, basi ninyongwe kwa haki kwamba niliua bila kukusudia, kwa sababu ni ajali tu ilitokea," alidai Luwonga.

Hapo Hakimu Rugemalira akaingilia akisema: "Unaanza kuhubiri sasa, wewe zungumza unachotaka kuzungumza ili nikiandike kwenye rekodi za mahakama."

Luwonga aliendelea kudai kuwa msingi wa kesi hiyo ni maelezo yake, baada ya kuwaambia polisi kwamba yeye ndiye aliyeua na ndiye aliyekuwa anajitumia ujumbe mfupi kutoka simu ya mkewe kwenda katika simu yake.

"Kama shetani angeendelea kunishikilia hadi leo hii, hakuna mtu angejua kitu nimefanya, lakini roho mtakatifu alinishukia na nilikuwa na sukumwa kusema ukweli. Kwa sababu nilikaa miezi miwili na siku moja bila ukweli kujulikana, hadi sasa Naomi asingejulikana yuko wapi.

"Kutokana na hofu ya Mungu, niliamua kusema ukweli sio kwa sababu nilipata mateso kutoka kwa askari polisi, hapana! Ni mimi mwenyewe niliamua," alidai Luwonga.

Mshtakiwa huyo pia aliiomba mahakama kuwa pindi kesi itakapoanza kusikilizwa, Mahakama Kuu ihamie sehemu ya tukio nyumbani kwake, ili waone mashimo sita aliyoyachimba katika nyumba zake sita na nyumba ya kulala wageni kwa ajili ya maji taka.

Alidai kuwa lengo la mahakama kwenda eneo hilo ni ili ione mashimo yaliyochimbwa yalikuwa ni ya maji taka na sio kwa ajili ya kumzika mkewe , kwa sababu yeye ndiye alitaka kwa ajili ya maji machafu.

Ni madai yaliyomfanya hakimu aingilie, akisema: "Sasa mshitakiwa huko unapokwenda ni kwenye ushahidi. Hayo utayazungumza huko Mahakama Kuu katika ushahidi wako."

Mshitakiwa Luwonga alidai: "Mheshimiwa ninaomba ufahamu jambo moja; hawa mawakili wangu nimewaomba wanitetee kwa haki na siyo kupindishapindisha mambo kwa sababu mimi ndiye niliamua mwenyewe kuzungumza ukweli," alidai Luwonga.

Alidai hayo baada ya wakili wake, Mohamed Majaliwa kumtaka aache kuzungumza. Wakili huyo alimtaka wazungumze kwanza wao kabla ya yeye kuendelea kuzungumza mbele ya hakimu.

"Ninawaomba mawakili wa serikali, mnipelekee taarifa zangu kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kwamba aharakishe kesi hii iishe haraka kwa sababu hata Rais na jamii kwa ujumla wanataka kujua mwisho wake kwa sababu kesi yangu hii ilitikisa nchi.

"Ninataka kesi hii iwe fundisho kwa watu wengi, kwa sababu tulifanya uzembe mkubwa sana sisi wanandoa na jamii pia ilifanya uzembe hadi mauaji yakatokea," alidai Luwonga.

Baada ya mshitakiwa kudai hivyo, Hakimu Rugemalira alimweleza kwamba hakuna kesi kubwa. Zote zinalingana na hakuna kesi inayotikisa nchi, hivyo hata kesi inayomkabili "sio konki" kama alivyodai.

Mshitakiwa huyo alidai atakuwa na mashahidi 20 na atakuwa na vielelezo wakati ushahidi unaendelea. Atavitoa mwenyewe au mashahidi wake watakuja navyo mahakamani.

"Una haki zako za msingi za kupewa wakili na kupewa orodha ya mashahidi, kama utahitaji na mawakili wako hawa wawapo, hilo ni jukumu lako wewe. Kwa hiyo, unahamishiwa kwenda Mahakama Kuu," alisema Hakimu Rugemalira.

Luwonga anadaiwa kumuua mke wake Naomi kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na baadaye alichukua majivu ya mwili wa marehemu na kwenda kuyafukia shambani kwake Mkuranga mkoani Pwani.

# Matumizi ya umeme yaongezeka nchini

**Na Maulid Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) limesema matumizi ya umeme nchini yameongezeka, likibainisha kuwa kwa mwezi Juni mwaka huu, matumizi ya nishati hiyo kilifikia megawati 1,470 na kiwango hicho ambacho kilikuwa hakijawahi kufikiwa.

Mkoani Dar es Salaam jana na Mhandisi Mkuu wa Mipango ya Uendeshaji wa Gridi ya Taifa, Zubeda Chuma, alibainisha katika maonyesho ya biashara ya kimataifa ya 47 yanayofanyika katika Viwanya vya Sabasaba.

Kwa sasa TANESCO wana vyanzo mbalimbali vya uzalishaji wa umeme ikiwamo mitambo inayotumia maji ambayo inazalisha megawati 574.60, gesi MW 1,148.82, mafuta MW 88.13 na tunganotaka MW 10.50, ambazo kwa ujumla ni MW 1822.05.

Alisema mwenendo wa matumizi ya nishati ya umeme umekuwa ukibadilika asubuhi na mchana, akifafanua kuwa nyakati za jioni, matumizi ya umeme huongezeka zaidi.

Alisema shirika limeendelea kuhakikisha linaimarisha vyanzo vyake vya uzalishaji wa nishati hiyo ili kuwa na umeme wa uhakika.

"Kwa siku huwa tunategemea matumizi ya umeme yanakuwa makubwa. Kwahiyo kama TANESCO tunahakikisha kwa nyakati ambazo matumizi yanakuwa makubwa, tunazalisha zaidi ili kukidhi mahitaji ya wateja," alisema na kuongeza:

"Kwa saa 24 ya siku kuanzia saa nne asubuhi mpaka saa nane mchana, tunapata mahitaji ya juu, lakini mahitaji makuu ndani ya siku tunayapata kuanzia 12 jioni mpaka saa nne usiku. Pia tunajua ndani ya wiki ni siku zipi mahitaji yanakuwa ya juu, ili tujiandae kuwahudumia wateja kwa ufanisi." alisema Zubeda.

Aliongeza kuwa ndani ya siku saba za wiki, siku ya Jumapili mahitaji hushuka tofauti na miaka nyuma ambayo mahitaji yalikuwa yanashuka kuanzia Jumamosi lakini kutokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kimaendeleo mwenendo wa matumizi umebadilika.

Alibainisha kuwa kwa kipindi cha mwaka mzima, kuna miezi ambayo mahitaji yanakuwa chini ikiwamo Machi hadi Juni kutokana na kipindi hicho kuwa cha mvua.

Vilevile, alibainisha kwamba ili kuendelea kutoa huduma bora, TANESCO huhakikisha kabla ya kufikia miezi ambayo mahitaji ya umeme yanakuwa juu, mitambo ya uzalishaji umeme inafanyiwa marekebisho ili kuwa tayari kwa ajili ya kuzalisha nishati inayokidhi mahitaji ya wateja wao.

Aliwakaribisha watanzania kutembelea katika banda lao katika Viwanja vya Sabasaba ili wajifunze masuala mbalimbali ikiwamo kuona namna umeme unavyozalishwa na kuona maendeleo ya miradi ya kuzalisha umeme, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP).

# TIRA: Una shida katika bima, njoo tuitatue

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) imewataka waliopata shida katika bima na hawajapata msaada, wajitokeze ili wapatiwe haki zao.

Meneja wa Kanda ya Mashariki wa TIRA, Frank Shangali, alitoa rai hiyo jana katika maonyesho wa biashara ya 47 ya kimataifa, maarufu Sabasaba yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Dar es Salaam.

Shangali alisema katika maonyesho hayo wamezikutanisha kampuni 33 zinazotoa huduma za bima, hivyo wenye malalamiko yoyote wajitokeze katika banda lao wapewe msaada.

"Malalamiko ambayo wananchi hawakuridhishwa na huduma kwa namna moja ama nyingine tutawasaidia kupata suluhu ndio maana tupo hapa na kampuni zote zinazotoa huduma za bima na watapata fursa ya kupata elimu ya bidhaa zinazotolewa na bima," alisema.

Meneja huyo alisema TIRA ni wasimamizi wa bima, hivyo wajibu wao ni kusimamia malalamiko na kuhakikisha walaji wa bima wanapata suluhu katika kampuni hizo za watoa huduma.

Shangali alisema malalamiko mengi wameyapokea ofisini na kwenye maonyesho ya Sabasaba yakielekezwa kwa kampuni za bima.

Alisema wamebaini kuwa malalamiko mengine yanatokana na kukosekana kwa uelewa wa namna ya kuwasilisha nyaraka kwa kampuni husika.

"Tumewaelimisha namna ya kuwasilisha matatizo yao katika kampuni husika wanaopata shida ili zitatuliwe kwa wakati na kuendelea kufurahia huduma za bima," alisema Shangali.

Alisema soko la bima linakuwa kwa kasi na kufikia asilimia 1.68 kulingalishwa na miaka ya nyuma lilipokuwa chini ya asilimia moja, hivyo wataendelea kutoa elimu kwa wananchi wawe na uelewa kuhusu umuhimu wa kutumia bima.

Alisema mwaka 2022 kumekuwa na ongezeko la biashara, hivyo kuchochea huduma za bima kuongezeka. TIRA imejipanga kuwalinda walaji wa bima na kupatiwa haki zao inapotokea amepata shida yoyote.

Alisema changamoto iliyopo ni uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya bima na baadhi kupotosha. Mikakati yao ni kuhakikisha sekta hiyo inakua kwa kasi na kuongeza uchumi wa nchi.



Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani ya Taasisi ya Umoja wa Amani Kwanza inayojishughulisha na maswala ya amani kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Mwarami Mitete (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu taasisi hiyo kupandisha bendera yake kwenye Mlima Kilimanjaro Julai 23 mwaka huu ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Kulia ni Makamu Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Joseph Mutakangarwa na Katibu wa Kanda ya Pwani, Upendo Nadeiti. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Hatimaye nyumba za mradi Morocco Square zakabidhiwa

**Na Romana Mallya**

HATIMAYE serikali imewakabidhi nyumba wapangaji na wanunuzi waliozinunua katika mradi mkubwa wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) wa Morocco Square ulioko Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

Mwezi Juni mwaka 2021, Nipashe iliripoti kuhusu kusimama kwa mradi huo kwa miaka minne. Ulianza kutekelezwa Juni 2014, ukitarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2017.

Mradi huo ulisimama mwaka 2017 baada ya ujenzi wake kuanza kusuasua mwaka 2015 kutokana na kupungua kwa wanunuzi wa mauzo ya kabla ya jengo kukamilika.

Akizungumza katika halfa ya makabidhiano ya nyumba kwa walionunua na kupanga ndani ya mradi huo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alisema Rais Samia Suluhu Hassan amechangia kwa kiasi kikubwa kuwezesha kukamilika kwa mradi huo.

"Niwapongeze sana NHC kwa kuuza nyumba 43 kati ya nyumba 100 zilizopo katika mradi huu. Wale ambao walichelewa au kusitasita kufanya uamuzi wa kununua nyumba za mradi huu, fursa bado ipo wanatakiwa kuwahi," alisema.

Waziri huyo pia alisema kuwa kati ya maduka ya biashara 52, tayari vyumba 49 vimeshapata wapangaji, akihamasisha wafanyabiashara wanaotaka kupanga wachangamkie vilivyobaki.

Aliipongeza NHC kwa kupata mwekezaji wa hoteli ya nyota nne ambayo ni sehemu ya jengo hilo.

"Mradi huu ni mkubwa. Miradi ipo lakini siyo iliyobeba huduma zote katika sehemu moja, niwapongeze NHC kwa ubunifu wenu katika uwekezaji wenye manufaa. "Morocco Square una sifa za kipekee sana, ikiwamo kuwezesha wateja wetu kuwa na eneo moja mtu anaweza kufanya shughuli zake zote. Mradi huu upo katikati ya mji, una huduma zote za kibinadamu," alisema.

Waziri huyo alisema yote ni jitihada ambazo zinahitaji pongezi kwa NHC na Rais Samia kwa kufungua milango ya uwekezaji.

"Shukrani hizi pia bado tunasema tumpe maua yake Mama Dk. Samia kwa sababu yeye ndiye kafungua mambo yote haya. Rais atakuja kuzindua nyumba hizi.

"Mradi huu ni kielelezo cha uboreshaji wa jiji kwa kuondoa majengo chakavu na kujenga ya kisasa yenye huduma zaidi ya moja. Mkurugenzi amesema hapa kulikuwa na nyumba mbili za makazi kabla ya mradi huu," alisema.

Alikumbusha kuwa mwaka jana, serikali ilizindua sera ya ubia ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje na pia sera ya ardhi ambayo mwanzo ilikuwa inazuia watu wa nje kutowekeza.

Waziri Mabula alisema mchakato wake wa kufungua fursa hiyo unaendelea ili waweze kuchukua (ardhi), wajenge nyumba na kuuza.

"Kwa diaspora pia, kuna utaratibu ambao umewekwa wa kutambulika kwa hati maalum, Rais amefungua milango wanaruhusiwa kuja kuwekeza kwa namna watakavyoona inafaa.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaandaa sera itakayowezesha diaspora kuwekeza katika ujenzi na kununua nyumba zitakazojengwa na NHC na waendelezaji wengine.

"Wenzetu wa Kariakoo waliokuja hapa, walipata taharuki kidogo waliposikia kwamba tuna wawekezaji wanaoingia ubia na NHC kuwekeza Kariakoo. Walipoelewa somo wao sasa ni mabalozi," alisema.

Waziri alitoa wito kwa watanzania wote wanaoishi nje ya nchi, kuja kuwekeza katika sekta ya nyumba.

Aliwaomba wakazi katika mradi huo wahakikishe wanatunza miundombinu yote ili idumu kwa muda mrefu.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah, alisema walionunua na kupangisha nyumba wako katika maisha tofauti kwa kuwa mradi huo ni ghali kuliko miradi yote wanayoitekeleza kutokana na kuwa na vifaa vyenye ubora wa hali ya juu.

"Tuko katika mradi wa kipekee na wanunuzi na hata wapangaji hawawezi kujutia kupanga ama kununua nyumba katika majengo haya ya Morocco Square," alitamba.

Mmoja wa wateja wa NHC, Aboubakar Aboubakar, alishukuru serikali na NHC kwa kufanikisha mradi huo na kuwataka wananchi kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo.

"Ni wajibu wa sisi wananchi kushirikiana na serikali kwa kwenda pamoja ili tupate maendeleo na NHC imekuwa wasikivu na nimeridhika na kazi inayofanywa na shirika hilo," alisema Aboubakar.

## HABARI KITAIFA



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde (wa pili kulia), akitoa maelekezo baada ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Shule ya Sekondari Mwanzi, wilayani Manyoni, mkoani Singida jana. **PICHA: TAMISEMI**

# MUHAS yaongoza ubora wa utoaji wa elimu Afrika

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

CHUO Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kimeshika nafasi ya kwanza kwa ubora Afrika Mashariki na ya tatu kwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara katika utoaji elimu ya juu.

Chuo hicho kimeshika nafasi hiyo kati ya vyuo 88 vilivyofanyiwa utafiti wa kina na taasisi ya utafiti ya Uingereza iitwayo Times Higher Education (THE) kwa kushirikiana na MasterCard Foundation katika nchi 20.

Utafiti huo uliopewa jina la 'The Sub-Saharan Africa Universities Rankings;, umefanyika kwa mara ya kwanza na taasisi hizo kutambua mchango wa vyuo vya elimu ya juu katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto katika jamii na kuleta ushindani wenye tija katika utoaji elimu ya juu barani Afrika.

Matokeo ya utafiti huu yaliyotangazwa mapema wiki hii, yalizingatia mbinu zinazotumika katika ufundishaji, uhusishwaji wa wanafunzi kinadharia na kivitendo katika masomo, uwezo wa chuo kifedha, uwazi katika udahili na haki katika utoaji elimu na mchango wake Afrika.

Kwa Afrika Mashariki, MUHAS inafuatiwa na Chuo Kikuu cha Makerere cha Uganda, UGHE (Rwanda), ARDHI (Tanzania), Embu (Kenya), UDSM/Mlimani (Tanzania) na Rongo (Kenya).

Kwa Bara la Afrika, vyuo vilivyotambuliwa kuwa na ubora wa hali ya juu viliongozwa na Chuo Kikuu cha Witwatersrand cha Afrika Kusini, alichosomea mpigania uhuru maarufu duniani, Nelson Mandela.

Cha pili ni Chuo Kikuu cha Johannesburg cha Afrika Kusini na cha tatu ni MUHAS cha Tanzania.

Vyuo vingine vya Tanzania vilivyotambuliwa kwa ubora kusini mwa Jangwa la Sahara ni: Chuo Kikuu cha Ardhi kilichoshika namba 10 na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichoshika namba 21.

Mwenyekiti wa Baraza la MUHAS, Dk. Harrison Mwakyembe, aliwambia mwandishi jana kuwa wamezipokea taarifa hizo kwa furaha na shauku ya kufanya vyema zaidi.

# Msonde aelekeza jicho katika malezi watoto elimu ya awali



**Na James Mwanamyoto**

NAIBU Katibu Mkuu (Elimu) Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Charles Msonde (pichai), amewataka walimu wa elimu ya awali kuhakikisha wanawapatia watoto malezi bora na ujuzi ili wakianza darasa la kwanza wawe na msingi mzuri wa elimu.

Dk. Msonde alitoa rai hiyo kwa walimu wote shule za awali nchini alipofungua mafunzo ya walimu 105, maofisa elimu kata 21 na walimu wakuu 21 wa Mkoa wa Singida. Mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha kutoa elimu yenye tija kwa watoto.

Alisema serikali inathamini elimu ya awali na ndio maana kupitia mradi wa BOOST, madarasa ya awali 12,000 yatajengwa ili kuwezesha shule zote za msingi nchini kuwa na madarasa ya awali. Alisema kuwa katia ya shule zote takribani 17,000 zilizopo, baadhi tayari zina madarasa ya awali.

"Elimu ya awali inajenga msingi bora wa malezi ya mtoto, tabia nzuri na utamaduni wa mtoto kupenda shule, na ndio maana Mheshimiwa Rais aliridhia mradi wa BOOST utengewe Sh. trilioni 1.15 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa mradi huu," Dk. Msonde alifafanua.

Aliongeza kuwa mradi huo umetoa fursa kwa walimu hao kujengewa uwezo wa kutoa mafunzo kwa watoto kulingana na hatua za makuzi.

Kiongozi wa wawezeshaji, Dk. Fortunata Pembe, alisema kuwa pindi walimu hao wakihitimu mafunzo hayo, watayatoa mafunzo kwa walimu wengine.

Mwalimu Mkumbo ambaye ni miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo, alishukuru kwa kupatiwa mafunzo na kuahidi kuyatumia vizuri ili watoto wa pate malezi bora na ujuzi.


## IN LOVING MEMORY OF LATE CRISPIN S.E. MWANYIKA



Job 19:25-26 **"For I know that my Redeemer lives, and at the last he will stand upon the earth. And after my skin has been thus destroyed, yet in my flesh I shall see God."**

It is now 24 YEARS since the lord called you home on 2.7.1999; you are remembered and deeply missed by your loving wife Jane, children- Nancy, Geoffrey, Mary & David, In-laws, Grandchildren, Brothers & Sisters, Relatives & Friends. There are special people in our lives who never leave us, even after they are gone. Always in our hearts always loved till eternity

***THERE WILL BE A REQUIEM MASS AT ST NICHOLAUS ROMAN CATHOLIC CHURCH, MTONGANI- KUNDUCHI BEACH ON SUNDAY 02.07.2023 AT 9.00AM.***

Ecclesiastes 3:1-2 ***For everything there is a season, and a time for every matter under heaven: a time to be born, and a time to die; a time to plant, and a time to pluck up what is planted***

***MAY THE ALMIGHTY GOD REST YOUR SOUL IN ETERNAL PEACE. AMEN.***

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunaunga mkono kuundwa kamati uchunguzi kifo cha mwosha magari

**KATIBA** ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaelekeza katika Ibara ya 14 kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.

Ibara ya 13 ya Katiba hiyo inapiga marufuku mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho alipokitenda hakikuwa kosa kisheria, hali kadhalika ikiainisha miongozo ya viwango vya adhabu kisheria kutozidi uhalisia.

Inaelekezwa katika ibara hiyo kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binadamu, heshima ya mtu itatunzwa katika shughuli zote zinazohusu upelelezi na uendeshaji wa mambo ya jinai na katika shughuli nyinginezo ambazo mtu anakuwa chini ya ulinzi bila uhuru au katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu.

Katiba ya nchi pia inapiga marufuku mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha.

Vilevile, inaporejewa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, kifungu chake cha 7(3) kinaelekeza kuwa pale mtu anapokufa akiwa mahabusu ya polisi au katika hospitali ya magonjwa ya akili, ukoma, makazi ya walemavu au gerezani, ofisa ambaye alikuwa amemweka mtu huyo kizuizini au aliyekuwa msimamizi wa sehemu hiyo, atatakiwa wakati huohuo atoe taarifa inayohusiana na kifo kwa korona wa mahakama mwenye mamlaka ya eneo ambapo mwili umekutwa na korona huyo au mtu aliyeruhusiwa.

Katika toleo la Nipashe la jana, kulikuwa na habari kuhusu madai ya familia ya kijana Mandela Petro (26), mkazi wa Mtaa wa Zambia, Kata ya Malampaka wilayani Maswa mkoani Simiyu, ambaye kifo chake kimezua utata.

Inadaiwa kuwa kifo cha kijana huyo kilitokea Juni 11 mwaka huu, huku chanzo chake kikizua utata - kuna madai ya ndugu zake kwamba aliuawa kwa kipigo toka kwa askari polisi wawili kwa tuhuma za wizi, pia madai ya kushambuliwa na wananchi wenye hasira kwa tuhuma za wizi.

Ni tukio ambalo Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Aswege Kaminyoge, amebainisha kumeundwa kamati ya uchunguzi ili kujua ukweli kuhusu chanzo cha kifo cha kijana huyo ndipo hatua zaidi zichukuliwe kwa mujibu wa sheria.

Nipashe Jumapili tunaunga mkono uamuzi wa kuundwa kamati ya kuchunguza kiini cha kifo cha kijana huyo kutokana na utata uliojitokeza.

Jeshi la Polisi limekuwa linanyooshewa kidole kutokana na baadhi ya askari wake kukosa weledi katika utekelezaji wa majukumu yao, hivyo kusababisha vifo na majeruhi kwa watuhumiwa wa makosa mbalimbali.

Vilevile, kumekuwa na matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi kwa kuwashambulia kwa silaha za jadi na hata kuwaua watuhumiwa wa makosa mbalimbali badala ya kuwafikisha katika vyombo vya dola kwa ajili ya hatua ya kisheria.


Mnamo Agosti 25, 2021, Rais Samia Suluhu Hassan aliwaonya askari wa Jeshi la Polisi kwa marejeo ya kina kuhusu madhila, hata vifo vya watuhumiwa mikononi mwa polisi.

Pia, ripoti ya mwaka huo (2021) ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ilibainisha mwaka ulikuwa na matukio sita ya utesaji na kutendwa isivyo haki kwa raia na vyombo vya dola. Ni matukio yaliyoripotiwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Dar es Salaam na Mara.

Nipashe tunaunga mkono uamuzi wa kuundwa kamati ya kuchunguza kiini cha kifo cha kijana Mandela mkoani Simiyu ili hatua zichukuliwe dhidi ya waliohusika, hivyo kuongeza uwajibikaji katika kusimamia haki za binadamu nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# DCEA ipewe ushirikiano udhibiti dawa za kulevya

Na Sabato Kasika

**MAMLAKA** ya Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA) imeepusha watu milioni tano katika matumizi ya dawa za kulevya huku ikikamata watuhumiwa 109 wakiwa na dawa hizo.

Baadhi ya dawa zinazotajwa kunaswa na mamlaka hiyo ni heroin, cocaine, bangi kavu, mbichi, iliyosindikwa na kuteketeza ekari 1,093 za mashamba ya dawa hizo katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lyimo, kiasi cha heroin kilichokamatwa kati ya Machi 25, 2023 hadi Juni 19, 2023, iwapo kingeingia sokoni, kingetumiwa na kuathiri watu milioni 4.815.

Kwa kuzingatia takwimu hizo, ni wazi ipo haja kwa watanzania kuwapa ushirikiano DCEA katika vita hivi ili washinde, hasa kutokana na ukweli kwamba dawa hizo zinaathiri Taifa la kesho.

Sidhani kama kuna mtanzania anaunga mkono biashara hiyo haramu iendelee.

Hivyo ni vyema tutoe ushirikiano kwa mamlaka husika kwa kutambua kuwa vita hivyo vinahusisha jamii nzima.

Katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani yaliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan alisema Tanzania imefanikiwa kuzuia uingizaji wa dawa za kulevya kwa asilimia 90. Lakini sasa dawa za kienyeji kama bangi zimeendela kuwa tatizo nchini.

Kwa kutambua hilo, ninadhani sasa ni vyema kushirikiana na mamlaka hiyo ya serikali ili asilimia 10 iliyobaki iishe na kuwa na asilimia sifuri ya matumizi ya dawa za kulevya nchini mwetu.

Watumishi wa umma waweke uzalendo mbele ili kusimamia maslahi ya Taifa kwa kutojihusisha kwa namna yoyote na biashara ya dawa hizo, ili kuokoa kizazi kijacho.

**Katika toleo la Nipashe la jana, kulikuwa na habari kuhusu madai ya familia ya kijana Mandela Petro (26), mkazi wa Mtaa wa Zambia, Kata ya Malampaka wilayani Maswa mkoani Simiyu, ambaye kifo chake kimezua utata.**

Ninasema hayo kwa kuwa hata Rais mwenyewe katika maadhimisho hayo alitoa rai kwa Jeshi la Polisi kutowabambika wananchi kesi, bali watende haki ili kuepuka chuki kwa wananchi.

Wazazi na walezi nao hawana budi kusimamia vyema majukumu yao, huku viongozi na jamii nao wakishirikiana na viongozi wa mila ili kusaidia kusimamia maadili mema.

Rais alifafanua siku hiyo kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 24 .41 kwa ajili ya kuwezesha mapambano na hatimaye kumaliza balaa hilo linalotokana na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

Ninadhani 'tungezionea huruma fedha hizo', kwa kushirikiana na serikali katika vita hii. Tutoe taarifa ni wapi zinakouzwa dawa za kulevya au zinaingizwaje, ili kusaidia kudhibiti uingizwaji na matumizi yake.

Hayo yakifanyika, inawezekana tukaokoa fedha hizo, zitakatumika kwa shughuli za maendeleo ya nchi. Bila ushiriki wa jamii kwa kutoa taarifa, ni wazi matumizi ya dawa hizo yataendelea kuwapo na hivyo kusababisha serikali kuendelea kutumia gharama kubwa kuwahudumia waathirika.

Ikumbukwe kuwa utafiti uliofanywa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na DCEA, umebaini kuwapo tatizo lingine kwa wavutaji wa shisha.

Kwa mujibu wa utafiti huo, watumiaji wa shisha huchanganya dawa za kulevya aina ya heroin na cocaine na kuchangia kuwapo kwa ongezeko la biashara za dawa za kulevya.

Inaporejewa taarifa ya DCEA kwamba vijana wanaojihusisha na matumizi ya dawa hizo ni wa umri wa kuanzia miaka 11, ambao kimsingi ni Taifa la baadaye, hatuna budi kuipa ushirikiano DCEA katika udhibiti wa dawa za kulevya nchini.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Pongezi kwa TLS katika hili la Bandari, kipi muhimu zaidi - Katiba, Bandari?



Pascal Mayalla

**TLS hawakuyaona yale niliyoyaona mimi!. Tanzania ni nchi, inakwenda kuingia mkataba wa kimataifa wa nchi na nchi, yaani Tanzania na UAE, lakini watia saini wa Tanzania ni nchi halali kimataifa, ila watia saini wa UAE ni kampuni ya DPW!**

NIKIWA mwanachama wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), nimeisoma taarifa ya TLS kuhusu suala la Bandari na DPW. TLS inastahili pongezi za dhati!

Ni kama imeufunga huu mjadala kwa upande wa hoja za kisheria, kwa kuainisha vipengele vyenye matatizo, kuonyesha tatizo ni nini na kushauri jinsi ya kurekebisha.

Kama ningekuwa kule 'Unyamwezini', hii inaitwa "funga kalomo", yaani funga mdomo! Taarifa hii ya TLS imefunga kazi kwa hoja za kisheria, hongera sana TLS kwa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa na huu ndio uzalendo!

Nikiwa mwanachama hai na mwaminifu wa TLS, kwa heshima ya chama changu cha wanasheria, ninaomba nisikosoe jambo lolote katika taarifa ya TLS, ila sio vibaya kuzungumzia baadhi ya hoja ambazo TLS haikuzigusia kabisa!

Ni baada ya kuisoma taarifa ya TLS, ndipo nikagundua kwamba kumbe mtu kusomea fani nyingine kwanza kabla ya kusomea sheria, kunakufanya kuwa na upeo mpana zaidi kuliko wanaosomea sheria pekee.

Ndio maana kule Marekani huwezi kusoma sheria moja kwa moja, lazima usomee fani nyingine kwanza ndipo uje kusomea sheria.

Mimi kabla ya kusomea sheria nimesomea uandishi wa habari kwanza, ndipo nikasoma sheria. Unajikuta unakuwa na jicho kali zaidi kuliko jicho la kawaida la mwanasheria aliyesomea sheria tu.

Jicho la mwanasheria linaangazia vifungu vya katiba, sheria, taratibu na kanuni tu, wakati jicho la mwandishi wa habari linaangalia mtazamo mpana zaidi wa mahitaji ya jamii, mwananchi wa kawaida, anaona nini, anataka nini, hivyo jicho la mwandishi wa habari mwanasheria linaona kuliko jicho la mwanasheria mwanasheria!

Baada ya Bunge letu kuridhia, niliandika makala 'Japo Bunge limeridhia, DPW kuendesha Bandari zetu, ni makubaliano tu, tukithibisha kuna matatizo, tunarekebisha mkataba wa HGA, kazi nzuri Iendelee!' Humo niliainisha upungufu wa IGA hiyo kisheria kwa jicho la kiuandishi wa habari.

TLS katika taarifa yao, kuna maeneo mengi wamepita mulemule nilimopita mimi, ila lile kubwa kuliko, la "The capacity to contract", TLS wamelikwepa na kuliweka kiporo kusubiria wawasiliane na Dubai.

TLS hawakuyaona yale niliyoyaona mimi!. Tanzania ni nchi, inakwenda kuingia mkataba wa kimataifa wa nchi na nchi, yaani Tanzania na UAE, lakini watia saini wa Tanzania ni nchi halali kimataifa, ila watia saini wa UAE ni kampuni ya DPW!

Tena aliyetia saini kwa Tanzania ni Rais wa Tanzania, aliyekasimu mamlaka ya kutia saini kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, kupitia idhini ya kisheria iitwayo POA, (Power of Attorney) ambayo kwa Tanzania, Rais Samia ametia saini, lakini upande wa Dubai, hakuna idhini yoyote toka UAE! Hivyo, Tanzania kuingia mkataba wa kimataifa wa nchi na nchi na kampuni binafsi iliyojifanya nchi!

Kwa maneno mengine ni kampuni ya DPW imejigeuza ni nchi ya Dubai wakati ni kampuni binafsi. Siyo nchi! Dubai siyo nchi, nchi ni UAE! Nchi yetu haiwezi kuingia mkataba wa kimataifa wa kuridhiwa na Bunge letu kama mkataba wa kimataifa wakati watia saini ni kampuni na siyo nchi na hakuna POA yoyote ya UAE kuruhusu DPW kuingia mkataba huo wa kimataifa.

Nimeipongeza TLS kwa uzalendo kwenye hili, ila nikiri kuwa nimeshangazwa na umakini huu wa TLS katika hili la Bandari.

Sheria kuu kuliko zote nchini kwetu ni katiba, katiba ndio sheria mama, sheria nyingine yoyote inayokwenda kinyume cha katiba ni sheria batili! Kinachoibatilisha hiyo sheria yoyote kinyume cha katiba, ni katiba yenyewe!

Ubatili wa sheria batili yoyote unabatilishwa na katiba, Mahakama Kuu ikiisha tamka sheria fulani ni batili kwa kwenda kinyume cha katiba, moja kwa moja sheria batili hiyo inakuwa imebatilika kuanzia hapo.

Nimalizie kwa pongezi tena, TLS kwa hili la Bandari, ila kuna makubwa kuliko hili la Bandari, nini muhimu zaidi kati ya katiba, haki na Bandari?

TLS bado hamjachelewa!

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Zana za kidijitali zitatuongezea ajira



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Baadaye zikaja simu za mezani, za kukoroga, angalau safari zikapungua, mtu mmoja akapewa fursa ya kutoa taarifa kwa watu wengi iwezekanavyo akiwa eneo moja tu, lenye simu.**

ZAMANI tulipopata akili ya kujikimu kimaisha, tuliachana na kuishi kwa kuangua matunda na kuchimba mizizi, tukaanza kulima na kupanda mazao mbalimbali kwa ajili ya chakula.

Lakini kwa kuwa teknolojia nayo ilikuwa duni, tulilazimika kutumia zana duni na idadi kubwa ya watu kulima eneo kubwa la kujitosheleza kwa mazao ya chakula.

Vivyo hivyo, hata katika matibabu, tulipougua tulitumia mitishamba kujitibu. Tulilazimika kunywa dawa hizo nyingi mabakuli kwa mabakuli na kuamini kupona.

Unywaji huo wa dawa hizo haukuwa na kipimo, ila kama ulijisikia vyema basi ndiko kulikuwa kupona kwako na wala hakukuhitajika dozi ya kunywa asubuhi, mchana na usiku, bali kufakamia bakuli lako kitumbo ndi!

Na hata katika kilimo hicho, mazao tuliyopanda nayo hayakuwa yakizaa sana kutokana na teknolojia duni, hivyo pia kulazimika kupanda mimea mingi ili kuvuna chakula kingi mwishowe.

Lakini jinsi mabadiliko ya sayansi na teknolojia yalivyoingia katika jamii, mambo yakawa rahisi kutokana na zana za kisasa kupatikana, majembe ya mkono yakatupwa na nafasi ikachukuliwa na ya kukokotwa na ng'ombe; plau.

Hatimaye plau nayo ikapoteza maana, pale matumizi ya matrekta yaliposhamiri, maeneo makubwa yakalimwa kwa muda mfupi na watu wachache na hatimaye mazao mengi kupatikana sanjari na chakula.

Teknolojia ilipoingia kwenye matibabu, dawa za kisasa zikapatikana na kuanza kutumika kwa dozi. Watu walianza kumeza vidonge na dawa za maji kwa kijiko badala ya mabakuli.

Haikuishia hapo, enzi hizo tukituma taarifa kwa barua kutoka eneo moja kwenda lingine, kwa kutuma watu kabla vyombo vya usafiri havijaanza kutumiwa kama baiskeli, pikipiki, magari na majahazi.

Lakini pia hata taarifa zingine zikifikishwa kwa miguu, mathalan ndugu walipofiwa, walitumwa watu kusambaa maeneo mbalimbali kufikisha taarifa za msiba.

Baadaye zikaja simu za mezani, za kukoroga, angalau safari zikapungua, mtu mmoja akapewa fursa ya kutoa taarifa kwa watu wengi iwezekanavyo akiwa eneo moja tu, lenye simu.

Zilipokuja simu za mkononi sasa ndiyo kabisa, hakuna tena mtu kukoroga simu, hakuna mtu kusafiri kupeleka barua wala taarifa. Mambo yote yanaishia kwenye simu kiganjani.

Kwa kweli teknolojia imechukua nafasi kubwa katika jamii na kuwezesha mambo kufanyika haraka haraka na maendeleo kupatikana, ingawa kwa athari hasi kwa baadhi ya watu.

Mnakumbuka zamani mizigo ikipandishwa katika malori kwa kutumia vichwa vya watu? Lakini teknolojia ikaja kuondoa yote hayo na kuwezesha sasa mizigo kunyanyuliwa kwa winchi!

Zamani barabara tukikusanyana wanakijiji kuzichonga, ili kutuwezesha kutoka mahali fulani hadi kwingine na tukitumia watu wengi na kupoteza siku nyingi pia. Yalipokuja matingatinga, ikawa kazi rahisi, mtu mmoja tu akiendesha, amemaliza.

Kila jambo lina uzuri na ubaya wake, kama ilivyo teknolojia ambayo hata katika vita, imetuletea mabadiliko makubwa, kwamba hamkusanyani na pinde na mishale watu kibao kwenye uwanja wa vita kupambana.

Badala yake silaha za kisasa zinafanya mambo, kutoka masafa ya maelfu ya kilometa na kushambulia kwingine kwa mtu mmoja tu kubonyeza kitufe na kombora kulipuka.

Hivi sasa katika ulimwengu huu wa teknolojia na dijitali, mambo yanafanywa na watu wachache sana, kwa kubonyeza vitufe tu na mambo kusonga mbele kwa manufaa makubwa.

Inanikumbusha Mbunge Joseph 'Musukuma' aliyeshuhudia maajabu ya Dubai katika bandari ya kampuni kubwa duniani, yenye uwezo wa kila kitu kuhusu tasnia ya bandari, kampuni ya Dubai Port World (DPW).

Musukuma alishuhudia mwanadada akibonyeza kitufe na makasha kunyanyuka na kushuka, akithibitisha kuwa hakuona utitiri wa watu bandarini hapo, akasifu sana teknolojia. Lakini hatimaye akapongeza uamuzi wa kuwaleta DPW bandarini kwetu, kwamba wataongeza ajira.

Hakika uwekezaji nchini wa 'wachawi' hawa wa huduma za bandari duniani, utatusaidia sana Watanzania, kwani kwa kuleta teknolojia mpya bandarini kwetu ambayo haihitaji watu wengi, itaongeza ajira.

Kwa hatua kama hii, Watanzania tunapigapiga midomo sana kwanini, wakati neema inakuja? Kwani ajira zitakuwa nyingi, tutaongezeka kuzipata bandarini na kufanya kazi bega kwa bega na mashine ya kisasa tukijifunza kwayo! Niko paleee!

**Alamsiki!**

# Serikali yaikabidhi OSHA magari, vifaa vya ukaguzi

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, ameukabidhi Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) magari 13 na vifaa vya ukaguzi vyenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni mbili vilivyotolewa na serikali ili kuboresha utendaji wa taasisi hiyo.

Magari na vifaa hivyo vilikanidhiwa jana katika hafla maalum iliyofanyika katika Ofisi za OSHA Kinondoni, Dar es Salaam na kuhudhuriwa na menejimenti na watumishi wa OSHA.

Hafla hiyo ilifanyika sambamba na ufunguzi wa mafunzo kwa watumishi wapya 18 ambao wameajiriwa ikiwa ni mkakati wa kuendelea kuboresha utendaji wa OSHA.

Katika hafla hiyo Waziri Ndalichako alisema magari na vifaa hivyo vimenunuliwa ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa katika maadhimisho ya Mei Mosi mwaka huu yaliyofanyika kitaifa mkoani Morogoro. Mkuu wa Nchi alisema serikali imepanga kuongeza hadhi ya OSHA.

"Haya yote yanafanyika leo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa katika hotuba yake akiwa mgeni sasmi katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) 2023 yaliyofanyika kitaifa mkoani Morogoro.

"Mheshimiwa Rais aliahidi kununua magari 13 na kuajiri watumishi wapya 18 ili kuiongezea Taasisi ya OSHA uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake," alikumbusha Waziri Ndalichako na kuongeza:

"Kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), ninapenda kutoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwa Rais wetu Mama Samia kwa kutambua umuhimu wa Taasisi ya OSHA nchini na kuamua kwa dhati kuipandisha hadhi na kuipa uwezo zaidi wa kutekeleza jukumu lake la msingi la kulinda nguvukazi ya Taifa hili pamoja na mitaji ya wawekezaji kwa kuwezesha upatikanaji wa vyombo hivi muhimu vya usafiri, vifaa vya ukaguzi pamoja na kuongeza idadi ya watumishi."

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, uwezeshaji huo wa serikali kwa OSHA utaongeza kasi na hamasa katika kukamilisha mchakato wa nchi kuridhia Mikataba ya Kimataifa Na. 155 na 187 kuhusu masuala ya usalama na afya kazini pamoja na kufanikisha utekelezaji wa sera ya kuinua sekta ya biashara na uwekezaji nchini.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema magari na vifaa vya ukaguzi walivyokabidhiwa, vitarahisisha kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa majukumu ya msingi ya OSHA hususan ukaguzi katika maeneo ya kazi pamoja na uchunguzi wa afya za wafanyakazi.

Aliiomba serikali kuendelea kuijengea uwezo Taasisi ya OSHA kutokana na uzito wa majukumu iliyonayo ya kusimamia usalama na afya katika maeneo yote ya kazi nchini.

"Hivyo, kwa niaba ya menejimenti nzima ya OSHA, nirudie tena kukushukuru sana wewe binafsi na ofisi nzima ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa miongozo yenu ya kila mara na tunaomba utufikishie shukrani zetu za dhati kwa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza ahadi yake ya kutupatia watumishi pamoja na magari mapya," alisifu.

# Mbunge 'atinga' wizarani na wafadhili wa miradi ya maji

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amemwahidi Mbunge wa Ulanga, Salim Hasham, wizara itampa ushirikiano wa kina kuhakikisha Wilaya ya Ulanga inamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama.

Alitoa ahadi hiyo jana alipotembelewa ofisini kwake Dodoma na mbunge huyo akiwa na wafadhili kutoka Uswisi.

Wafadhili hao wametua nchini kwa lengo la kuangalia changamoto ya maji wilayani Ulanga ili kuona namna bora ya kuisaidia kuondokana na shida hiyo.

Waziri Aweso alisema wizara itahakikisha wilaya hiyo inakuwa na miradi mingi ya maji na kuisimamia ili ikamilike kwa wakati na hatimaye wananchi waondokane na shida ya maji.

Mfadhili wa miradi ya maji kutoka Uswisi, Rubab Jawad Aziz, alitaja kilichomvutia kusaidia Wilaya ya Ulanga kuondokana na tatizo la maji ni wazazi wake ambao waliishi huko, naye alilelewa huko.

Alisema anajua changamoto hizo za maji tangu akiwa mtoto mdogo kabla ya kwenda Ulaya kutafuta maisha, hivyo aliahidi atashirikiana na serikali kuwapatia wananchi wa maeneo hayo maji salama na ya uhakika.

Mbunge Salim alisema amekuwa anatafuta wafadhili kwa wingi ikiwa ni sehemu ya jitihada za kusaidiana na serikali kutatua changamoto mbalimbali za jimbo hilo, ikiwamo maji.

Kwa mujibu wa Wizara ya Maji, Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro inazalisha lita 8,000 hadi 9,000 za maji ilhali mahitaji ya huduma hiyo ya msingi ni lita 1,600,000.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo akizungumza na wachimbaji wa madini ya dhahabu, baada ya kutembelea migodi zaidi ya mitatu iliyopo Kijiji cha Kiegei, wilayani humo juzi, kujionea uharibifu wa mazingira unaofanywa na wachimbaji wadogo na wakubwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mil. 80/- za Mfuko wa Jimbo kuelekezwa sekta ya elimu

**Na Abdul Mitumba, LIWALE**

OFISI ya Mbunge wa Liwale mkoani Lindi imesambaza vifaa mbalimbali vya ofisini katika shule nne za msingi na sekondari pamoja na Kijiji kimoja ili kufanikisha ujenzi wa ofisi ya serikali ya kijiji.

Baadhi ya vifaa vilivyotolewa ni mashine nne za kudurusu nyaraka, matofali 2,000 ya kuanzisha ujenzi wa ofisi ya serikali ya kijiji, mabati 200 na mifuko 200 ya saruji, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 84.

Mbunge wa jimbo hilo, Zuberi Kuchauka (CCM), alimwambia mwandishi juzi wilayani hapa kuwa vifaa hivyo vimetokana na fedha za Mfuko wa Jimbo na vimetolewa kwa nyakati tofauti ili kuimarisha ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na kuimarisha utawala bora vijijini.

Alizitaja shule zilizonufaika na vifaa hivyo kuwa sekondari za kata za Kiangara, Nangando, Makata na Mirui, ambazo kila moja imepata mashine moja ya kuchapa nakala.

Alisema Shule za Msingi Mbonde na Nangano kila moja imepata matofali 1,000 ili kuanzisha ujenzi wa madarasa.

"Kwa upande wa mabati, 70 tumepeleka katika Kijiji cha Tepetepe, mabati 80 katika Zahanati ya Kijiji cha Nambinda na 50 yaliyosalia tumeelekeza kwa taasisi za dini," alisema.

Katibu wa Mbunge wa Jimbo hilo, Jaizu Mkinde, alithibitisha kusambazwa kwa vifaa hivyo na kufafanua kuwa thamani yake ni zaidi ya Sh. milioni 84.4.

"Ofisi ya mbunge pia imepeleka vitanda viwili na kuvikabidhi katika Zahanati ya Kijiji cha Kichonda. Kimoja ni cha kujifungulia na kingine cha kupumzikia," alifafanua.

Mkinde aliwaomba wanufaika wa vifaa hivyo kuvitumia kwa uangalifu na kwa mahitaji yaliyokusudiwa ili vidumu kwa muda mrefu na kuleta manufaa kwa jamii.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 4, 2023**

**MDAI: MARIYAM JUMA VUAI**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: SALUM KHAMIS HASSAN**

**KWA: SALUM KHAMIS HASSAN**

**POPOTE ALIPO**

**Ombi la mdai: ARIYAM JUMA VUAI**
**Madai ya TALAKA**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limapangwa kusikilizwa mnamo tarehe 03 Mwezi 07 Mwaka 2023 Saa 2:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuhudhuria / hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

**Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 26 mwezi 6, 2023**

KUPOTEA KWA CHETI



**SUMAIYA ABDULAZIZ MUAWIYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: S4384-0152 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SOMBETINI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/209303/2023**

# MAISHA

JUMAPILI JULAI 2, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14


**Jilambe na sambusa za nyama**



Ukurasa 14

## UREMBO:

Fahamu haya kuhusu rangi ya jeli




## KATUNI


Ukurasa 16




# Nani kakwambia mpaka uagize gauni la harusi

Ukurasa 12

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | | Z | U | N | G | U |
| S | | | | Y | | S |
| H | | M | T | O | | H |
| A | R | A | | K | A | A |
| M | | K | O | A | | M |
| B | | A | | | | B |
| A | G | A | N | O | | A |

## AMSHA AKILI


MALIZIA MCHORO HUU KWA KUUNGANISHA NUKTA KUTOKA NAMBA 1 MPAKA 30




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UMA, IGA, JANGA, JEMBE, BONGEA, JAMBIA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa akitembea juu ya sakafu ya marumaru kwa mwendo wa haraka, mama yake alimwangalia na huku akiwa na hofu asije akateleza na kuanguka chini.

Mama: Grace unakimbilia wapi, hujui kama unatembea kwenye marumaru?

Grace: Mama nakwenda kuchukua kitabu changu cha hadithi Juma ameniibia.

Mama: Lakini kuwa mwangalifu, usije ukaumia na mimi sina pesa ya kukupeleka hospitali.

Grace: Lakini mama kule shuleni mwalimu alitufundisha kwamba 'kuteleza si kuanguka', hivyo sina hofu.

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu alitaka kuwajenga muwe na ujasiri wa kufanya jambo ambalo awali umeshindwa.

**SWALI**

Taja aina tatu ya wanyama wa jamii ya swala wanaopatikana porini.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Ukifanya haya mama mkwe atakufurahia

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu kuhusu wakwe. Wiki iliyopita tulijadili baadhi ya mambo yatakayofanya mama mkwe akuchukie. Leo tuangalie yale ambayo utafanya ili mama mkwe awe na furaha na wewe.

Kwanza; ni muhimu sana ubadilishe mtizamo wako kuhusu hadithi ulizosikia kuhusu mama mkwe. Wengine wataambiwa mama mkwe ni mjeuri, mchoyo au ana majivuno.

Au haelewani na majirani, anamtawala mume wake, hivyo nawe atakutawala, mradi maneno ni mengi utakayosikia kukukatisha tamaa. Wengine hukuambia hivyo kutokana na kukuonea gere (wivu). Wanatamani kuolewa wao.

Wengi huamini kwamba wakwe zao ni wabaya au wachawi wakati siyo kweli. Nieleweke hapa kwamba sisemi hakuna mama mkwe ambao ni wachawi. Wapo walio na imani hizo, lakini siyo wote!

Kingine mke unapaswa kumwona mama mkwe kama mama yako mzazi na si 'mama yake'. Kwa maneno mengine wazazi wa mumeo ni wazazi wako pia.

Vilevile, jipe muda kumsoma mama mkwe kisha mpe anachohitaji. Dada mmoja akaniambia mama mkwe wake alimpigia simu akitaka amtumie fedha kidogo, akamwambia hana, japokuwa alikuwa nazo. Yaani alimnyima eti ni msumbufu.

Lakini akimpigia mama yake mzazi, haraka anamtumia fedha. Ubaguzi huu haujawahi kuleta afya katika ndoa. Unamnyima anachohitaji mama mkwe wako kisha unategemea akupende?

Huwa anajua kabisa kile anachokiomba kwako unacho ila unamnyima. Ili akupende, mpe kile anachokihitaji kadri ya uwezo wako. Pia mwonyeshe upendo.

Kingine unatakiwa kufungua moyo wako na uwe mwazi kwake maana yeye ni mzazi wako pia. Una tatizo usiliweke moyoni, mshirikishe aone namna ya kukusaidia katika kulitatua.

Usije ukaishi naye milele katika nyumba yake. Na kama itakulazimu uishi naye, basi ishi naye ndani ya nyumba yako. Mwingiliano na mama mkwe mara nyingi huleta mizozo.

Lipo jambo ambalo utakuwa unafanya na halimfurahishi, hivyo kukuonya. Lakini wewe unachukia, jambo ambalo litaondoa furaha kati yenu. Lakini ukiwa mbali kidogo naye, siyo rahisi kughadhabika. Ukiishi kwako utakuwa na faragha zaidi.

Kingine cha muhimu ili mama mkwe akufurahie, mpende mtoto wake, na mjulishe kuwa unampenda mtoto wake. Ukimlaumu au kumzungumzia vibaya mtoto wake, katu hatokupenda. Ongea mambo mema kuhusu mumeo mbele yake.

Jambo lingine la kuzingatia ni kwamba usithubutu kumwita mumeo kwa jina lake mbele ya mama mkwe. Maana kwa tamaduni za kiafrika itakuwa na tafsiri kwamba wewe haumheshimu mumeo.

Kingine mhudumie pale anapokuwa na uhitaji. Akiomba umfulie nguo zake usikaidi hasa endapo hakuna mfanyakazi wa nyumbani. Hapo anajaribu kupima upendo wako kwake.

Pia usiwe na matumizi mabaya ya fedha. Kuwa makini na jinsi unavyotumia fedha ukiwa unaishi na mama mkwe. Akiona unafanya matumizi makubwa yasiyo ya lazima, huwa hafurahii. Wakati mwingine akishindwa kuvumilia atakuuliza.

Ikitokea hivyo, usijibu kwa jeuri, msikilize hoja yake na utumie hekima kumjibu. Ikiwezekana mwombe msamaha na ujieleze kwa upole, usiwe mkali. Yeye ni mama. Anakufundisha jinsi ya kuwa na bajeti nzuri yenye tija.

Kingine usije ukamsema mumeo kwa ndugu zake. Kama lipo tatizo kaeni mlisuluhishe wenyewe, au nendeni kwa mchungaji wenu au kwa washauri wa ndoa na kadhalika. Lakini siyo kwa ndugu zake.

Elewa kuwa mumeo ni ndugu yao na kwa vyovyote vile watamwegemea ndugu yao na kumtetea kwa kile unachokizungumza juu yake!

Kingine pendelea kumpa zawadi kila mara. Usiwe mchoyo. Wakati wa sherehe za sikukuu mnunulie zawadi nyingi kadri ya uwezo wako. Mnunulie vitenge vizuri, mnunulie chakula na kadhalika.

Mpe huduma kwa umakini mkubwa. Mara zote hautaweza kuongea naye kama jinsi unavyoongea na mama yako mzazi au unavyomfanyia mama yako mzazi. Mama mkwe yeye anapenda kudeka wakati mwingine, kitu ambacho mama yako mzazi hawezi kufanya!

Msamehe pale anapokukwaza kwani hakuna mwanadamu aliyekamilika chini ya jua. Msamehe hata kama alihusika kupinga uchumba wako kwa mtoto wake. Msamehe kwa sababu hayo yamepita kwani alikuwa anafanya jukumu lake kumlinda mtoto wake.

**Mfurahie kwa yale mema hata kama ni machache anayokutendea. Anapokununulia zawadi ipokee kwa moyo wa shukrani. Tembea katika uwapo wa Mungu siku zote za maisha yako! Kwa leo tuishie hapa. Je, una maoni au kisa? Ujumbe mfupi 0715268581**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Kukua si namba, ni uwezo wako wa kutafsiri, kupima

AGOSTI 8, 2022, Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa ziarani mkoani Njombe, aliwaonya wateule wake kuhusu kujikweza. Badala yake watoe huduma kwa wananchi kulingana na viapo vyao.

Ninakumbuka vizuri aliposimama na kuwasalimu wananchi wa Kijiji cha Mayale, Wilaya ya Wanging'ombe, Rais Samia alisema "huku juu hakuna watawala. Kwa hiyo Mkuu wa Mkoa siyo mtawala, Mkuu wa Wilaya, hata Mkurugenzi ni watoa huduma kwa watu, na kama hawafanyi hivyo, mtuambie haraka sana, kwa sababu tumekula kiapo kutoa huduma kwa watu."

Akasema kama kuna kiongozi hatekelezi hayo, apewe taarifa ili achukue hatua kwa kuwa wamekula kiapo ili kuwapa huduma wananchi.

Kwa sababu, lengo ni Tanzania yote ipate maendeleo, inanyanyuka, watu wote wawe na furaha, uchumi ukue na maisha yaendelee.

Wakati tunakumbishana hilo, nimeona habari inayoeleza mgongano kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli mkoani Arusha na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo.

Hawa wanadaiwa kutofautina jambo dogo - kucheleweshwa makabrasha ya mkutano maalum wa Baraza la Madiwani lililoketi kujadili utekelezaji wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu na Serikali za Mitaa (LAAC).

Mwenyekiti wa Halmashauri anadaiwa kukasirishwa na kitendo hicho na kumshtaki Mkurugenzi huyo kwa Mkuu wa Mkoa, kwamba hayuko tayari kuruhusu kikao hicho kiendelee, kwa sababu hana uelewa wowote wa ajenda zitakazojadiliwa na madiwani wake, kwa kuwa makabrasha ya vikao amewekewa mezani asubuhi.

Alinukuliwa akisema "siko tayari kuendesha kikao ambacho ajenda zake sijazipitia, wala sizifahamu maana nilipewa taarifa za kikao kupitia simu ya kiganjani.

"Kibaya zaidi, nilimwita mkurugenzi asubuhi hii ili tujadili hizi ajenda akakaidi. Nikamtuma Ofisa Utumishi, amwite akakaidi. Mkuu wa Wilaya, akamwita akasema anakwenda hospitalini, lakini cha ajabu sasa ameingia kwenye kikao.

"Sisi Wamasai hatupendi dharau, dharau ni bora nikaukosa udiwani na Uenyekiti wa Halmashauri kuliko kudharauliwa. Na kama nina upungufu, ninaomba niambiwe upungufu wangu, lakini siyo kudharauliwa. Nilikuwa Mwenyekiti wa kipekee, ambaye ninatetea sana maslahi ya watumishi lakini sasa itabidi nibalike," alisema.

Nilichokipenda - Mkuu wa Mkoa ameona tatizo, amekemea na ameagiza baada ya kugundua halmashauri hiyo mbali na mgongano huo, pia inakabiliwa na tatizo katia ukusanyaji wa mapato chini ya makisio. Akaeleza namna alivyoshtukia mchezo mchafu wa baadhi ya watu waliopewa dhamana ya kukusanya mapato, kuchezea mfumo wa ukusanyaji mapato.

Mkuu wa Mkoa alisema "Mkurugenzi hali ya ukusanyaji wa mapato siyo mzuri katika Halmashauri ya Monduli. Lakini pia kuna mchezo wa kuchezea mfumo wa ukusanyaji mapato. Hali hii ndio inayosababisha hata vikao vya Halmashauri kutofanyika kwa miezi mitatu, huku kukiwa na madeni ya posho za vikao."

Kutokana na hali hiyo, akaagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, kuisimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, badala ya kutegemea ruzuku ya serikali kuu.

"...haiwezekani mtegemee ruzuku za kutoka serikali kuu, wakati huku mnachezea mfumo wa ukusanyaji mapato. Ifike wakati kila diwani asimamie miradi kikamilifu iliyoko katika kata yake, kwa sababu miradi hiyo siyo ya halmashauri, wala MKuu wa Mkoa.|"

Kuhusu malalamiko ya Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mkuu wa Mkoa, amenukuliwa akisema ameyapokea na amemuelewa vizuri, akimtaka awe na amani, na kumshauri aridhie kikao kianze kupitia hoja za CAG, kwa sababu ni wajibu wao kuhakikisha Monduli inasonga mbele, kwa sababu ni Wilaya yenye historia ya kipekee.

Ninajiuliza kama ndivyo! Watu hawa hawakumbuki onyo la Rais Samia akiwa Njombe? Nani amewaroga. Msinihukumu kwa hili ninalowakumbusha kuhusu onyo la Rais. Mimi ninaamini kukua si namba, bali ni uwezo wako wa kutafsiri, kupima na kuchambua vitu. Hebu tutoke huko bwana, tufanye kazi tuliyotumwa!

**Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**



**Nani kakwambia mpaka uagize gauni la harusi**

Siku hizi kuna mafundi wenye ustadi wa hali ya juu wa kushona nguo za harusi na ukatoka pambe. Hakuna haja tena ya kutoa oda na kusubiri nguo yako muda mrefu ni kwenda tu kwa madesigner wakupime na kukushonea.

Furahia siku yako ya harusi kwa kupunguza mlolongo wa vitu kama kuagiza nguo nje ya nchi.

Kama ambavyo maharusi wanavyoonekana kwenye picha hapa.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## FURAHIA JAKETI

## ONDOA KERO YA BARIDI

KATIKA kukabiliana na hali ya baridi la vuguvugu linalotokana na kipupwe, mavazi yanayoongeza joto yanahitajika kila wakati.

Kulingana na baridi la wastani vazi la jaketi lina umuhimu kwa kuuweka mwili sawa na hatimaye kuendelea kufanya shughuli zako bila usumbufu.

Kimsingi ndani ya nyumba ni muhimu kuwa na jaketi hasa aina ya puffer kwa sababu ni vazi lenye mwonekano mzuri, licha ya kubuniwa miaka mingi.

Hata hivyo, wabunifu wamefanya marekebisho mengi ili kuendana na wakati, kutokana na aina ya majaketi yenye kola ngumu hadi zisizo na kola au kuwekwa ndogo na laini.

Nguo za aina hii zilipata umaarufu kuanzia miaka ya 90, karibu kila mtu alivaa, baadaye likafanyiwa marekebisho na kuwa vazi la watu maalum hasa vijana wanaotaka kwenda na wakati.

Katika miaka ya 90 jaketi hizi kwa kawaida zilikuwa na kola, cuffs na maelezo tofauti kama vile muundo uliofupishwa wa Massimo Dutti uli-oonyeshwa hapo juu. Hata hivyo, leo mtindo ni kuweka kamari miundo rahisi kwa sauti moja na besi za mviringo kama Mango anorak kifuniko.

Sifa kubwa ya nguo hizi ni kuwa na uwezo wa kutengeneza joto wakati wa baridi na pia lina mwonekano wa kuvutia pale mtu anapovaa.

Aina hii ya majaketi hayachagui nguo zingine za kuvaa, mfano unaweza kuvaa na suruali ya jeans, suruali ya kitambaa au nguo ya mazoezi.

Usisahau ukitaka kupendeza zaidi pigilia viatu vyako vya kutumbukiza kama raba, buti na viatu vingine unavyopenda.

## UREMBO

Na Mary Geofrey

# Fahamu haya kuhusu rangi ya jeli



RANGI za jeli (Gel) zimechukua umaarufu mkubwa kwa sasa kutokana na kuwa jibu la kilio kikubwa cha rangi kutoka mapema.

Rangi hizi hudumu kwa muda wa wiki mbili hadi tatu kama zikitunzwa vizuri, tofauti na rangi za kawaida ambazo hukaa kwa muda mfupi.

Rangi ya jeli

Aina hii ya rangi imeundwa na methacrylate polymer, hii rangi hukaa muda mrefu katika kucha, hii ni sawa tu na rangi ya kawaida tofauti zake ni kwamba hii haikauki kawaida badala yake hukauka kwa kukaushwa na kifaa kinachotumia umeme.

Faida za jeli

Kama tulivyosema mwanzo rangi hizi huchukua muda kubanduka au kutoka, wakati mwingine hazitoki mpaka pale unapozichoka na kuamua kuzitoa mwenyewe.

Mambo ya kuzingatia

Rangi ya jeli husababisha kucha kuwa dhaifu na zimekuwa zikilalamikiwa kusababisha kucha za asili kudhoofika.

Inaweza kusababisha maambukizo ( Infections).

Wataalam wengine wanadai kuwa inachukua kucha karibu wiki sita kupona baada ya kupaka rangi ya jeli.

Pumzisha kucha baada ya kutoa rangi ya jeli, usitoe ukapaka tena hakikisha zinapumzika kwa muda wa wiki kadhaa kabla ya kupaka tena rangi hii, kuzipaka mara kwa mara unazidi kudhoofisha kucha zako za asili

Usikae nazo muda mrefu, uzitoe ndani ya wiki mbili hadi tatu usikae nazo zaidi ya hapo.

Unashauriwa usitoe rangi hii kwa kubandua hakikisha unaenda kwa mtaalamu azitoe.

Paka mafuta maalum ya kuzuia jua (Sunscreen) kwenye vidole vyako kabla ya kuingiza vidole vyako katika mashine za kukaushia, kulinda vidole vyako na mionzi hii ya kukaushia kucha.







## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Jilambe na sambusa za nyama

SAMBUSA za nyama hupendwa na wengi lakini wengi hawajui kuzipika.

Leo katika safu yetu ya mapishi tutaelekezana namna ya kupika sambusa tamu ambazo unaweza kunywa na soda, juisi, chai au maji.







**Mahitaji**

Nyama iliyosagwa nusu kilo na kijiko kimoja kikubwa cha chakula cha pilipili manga.

Kijiko kimoja cha chakula cha kitunguu Thomu na tangawizi iliyosagwa na mafuta ya kupikia kiasi.

Vijiko vinne unga ngano au ute wa yai kwa kufungia sambusa.

Kaki za sambusa au manda au chapati nyepesi (unaweza kununua zilizokuwa tayari zimeshakatwa kwa ajili ya sambusa au kama utanunua zile sheet pana utazikata kwa inchi 4 upana wa ruler yaani upate mistari 3.

**Jinsi ya kupika**

Kausha nyama ya kusaga kwa kitunguu swaumu (thomu) na tangawizi pamoja na chumvi mpaka ikauke vizuri iache ipoe.

Katakata majani ya kotmiri weka upande katakata upate vipande vidogo vidogo(chop) vya vitunguu maji.

Zikate pilipili zako vipande vya mviringo vidogo vidogo.

Wakati ukimaliza matayarisho haya na nyama yako itakuwa ishapoa kabisa hapo ndio utachanganya, binzari nzima pamoja na pilipili manga pamoja na vitu vyote ulivyokwisha vitayarisha.

Koroga unga ndani ya kibakuli au ute wa yai na weka kaki kwa mfungo wa pembe tatu kama kofia na weka mchanganyiko wa nyama yako kiasi na uanze kuzifunga sambusa zako na ukifika mwisho hapo ndipo upake unga wako kwa ajili ya kuifunga isifunguke wakati wa kuchoma, pendelea kutumia kaki mbili kwa kila sambusa moja.

Kuchoma kwake ikiwa unazifanya na kuzichovya hapo mafuta lazima yawe baridi (ninakusudia uweke mafuta na uzitie sambusa kabla hayajapata moto).

Na ikiwa uliziweka kwenye friji zikaganda basi unatakiwa uzichome kwa mafuta ya moto.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# KUWA MBUNIFU KUPANGA VITU NYUMBA YENYE NAFASI NDOGO

ASILIMIA kubwa ya wakazi wanaoishi mijini wanaishi katika nyumba za kupanga.

Na kutokana na hali halisi ya familia za kiafrika, ni chache ambazo huwa na uwezo wa kumudu kupanga nyumba yote au nyumba kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo za kiafrika, nyingi huwa zinajumuisha zile kama zinavyojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended family' na hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato kilichopo cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Hivyo, ili umudu kuishi katika nafasi ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia iliyopo, lazima ubunifu na akili nyingi itumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza kuweka ndani ya nyumba baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Katika uwekaji wa samani ndani ya nyumba hiyo ndogo ni lazima uhakikishe unaweka zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhi vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano meza ya televisheni unaweza kuweka ambayo inakuwa na matumizi ya kuwekea TV na pia kwa kuhifadhi vitu vingine hususani vitabu na vingine vya umbo hilo.

Tumia sehemu ya ukuta wako wa dari 'kudizaini' kwa ajili ya kuwekea vitu vingine kama mapambo na kama ni jikoni unaweza kujengea na kuweka vyombo na vitu vingine na likatumika kama kabati la kawaida la vyombo.

Kabla ya kutengeneza samani hizo, hakikisha kwanza umepima nafasi iliyopo na ni muhimu kuzingatia zaidi upangaji wa vitu vyako ndani uwe wa kutumia hesabu zaidi siyo kupachikapachika tu.

Epuka kuweka vitu ovyo, ikiwezekana panga ambavyo una uhakika ni vya muhimu zaidi.

Kwa viti au sofa, hakikisha unaweka ambazo hazichukui nafasi kubwa, kabla ya kununua au kutengeneza ni vyema ukapima nafasi ambayo umepanga kuziweka.

Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka samani zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa na ikiwezekana ziwe ni nyembamba zenye nafasi ya kuelekea juu na si kwa upana.

Usiweke kitu kwa kuwa umeona kwa jirani yako ameweka, isipokuwa kwa kuzingatia umuhimu wake na nafasi uliyonayo katika nyumba yako.

Pia, kwa sasa katika samani, kumekuwapo na mabadiliko makubwa, fedha ndio inaweza kuamua uwe nayo ya dizaini gani.



## Maajabu matano mapambo ya ndani mwaka huu



TUMEHITIMISHA ungwe ya kwanza ya miezi sita ya kwanza ya mwaka huu wa 2023 juzi. Leo ni siku ya pili kati ya siku 184 zilizosalia kumaliza mwaka.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wametoa orodha ya mwenendo wa mapambo ya ndani katika kipindi cha miezi sita iliyopita, wakieleza kuwa matumizi ya mbao, rangi tulivu, kuchanganya mwonekano wa kisasa na wa zamani na bustani ni maeneo yanayoendelea kushika kasi mwaka huu wa 2023.

Mtaalamu wa mapambo, Ndigwako Mwakyelu, anasema rangi ya bluu na kijani tulivu, ndizo zinazopendelewa zaidi mwaka huu huku nyeupe na nyeusi, zikitajwa kama rangi muhimu za kuongeza nakshi ndani ya nyumba.

Anasema mchanganyiko wa mapambo ya zamani na sasa hasa samani ni eneo linaloongeza mwonekano wa kipekee ndani ya nyumba na bustanini pia.


"Unaweza kuweka meza ya kula yenye mwonekano wa kizamani lakini picha za ukutani na meza ya bufee ikawa ya kisasa, huu ni mchanganyiko mzuri sana wa kupendezesha nyumba," anasema.

Ndigwako anasema mabadiliko ya tabia nchi yamegusa kipekee eneo la mapambo, hivyo hamasa imekuwa kutumia vitu vinavyotunza mazingira, kuanzia aina ya maua ya kupanda msisitizo ukiwa ni yale yanayosafisha zaidi hewa.

**DONDOO**

- Panda maua yanayosafisha hewa
- Tumia rangi tulivu hasa vyumbani
- Samani ziwe ni za mbao
- Taa zinazotumia umeme kidogo
- Acha matumizi ya plastiki

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
WEWE SIO MKE KWANINI HUKAUKI KUNIFATA OFISINI?
USHASEMA MIMI SIO MKE ULITAKA NIKU-FATE WAPI?
SINA NAMNA YA KUKUINGIZA NDANI 'MCHEPUKO' TAZAMA WANANGU BADO WAPO MACHO ITAKUWA DHARAU!
HII MITOTO LAZIMA UTAKUWA UMEZAA NA KOLOKOLONI HAIWEZEKANI SAA NANE USIKU WANACHEZA 'BAISHOO!'
UMEMUONA JAMBAZI NA SILAHA GANI?
SWALI HILO ATALIJIBU YEYE TUKIFIKA
MANENO YENU YA KWENYE DALADALA MSITULETEE HUMU! SISI WENGINE MBOGA SABA TUPO HUMU
MWANGALIE! 'MBOGA SABA' CHINI UNA NDALA VUMBI KIBAO NA DOMO KAVU!
BRAZA! HUMU TUNAPANDA WATU WA USWAZI TUNA STORI ZETU ZA KISWAZI
WAKISHUA PIA TUMO TUNAZIMISI STORI ZA USWAZI
WAKISHUA UTANGOTANGO NA MAPUNYE UTAZANI RAMANI YA DUNIA!
SIONI HATA MAANA YA NENO 'YAKALE NI DHAHABU' INGEKUWA FLATI FASTA SANA!
"NAWEKA BONDI NINA SHIDA BUKU TANO TU!"
USINILETEE NGONJELA ZAKO NAKWAMBIA UTANIUDHI UTAHAMA!
VIPI KUHUSU MASHAIRI MAMA YANAPANDA?
KAJICHUBUA KAPITILIZA SASA IMEBAKI NGOZI YA NDANI NDIO MAANA MWILI UMEKUWA KAMA KIDONDA!
DUH! RED MEET!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
UKITOA TALAKA KUNJUA ROHO, MUME MWENZIO ATAWALE...

## HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitembelea na kukagua maendeleo ya uboreshaji wa shughuli za Bandari ya Tanga, akiwa katika ziara ya siku moja mkoani humo, jana. **PICHA: OWM**

# Kamati utaratibu mpya mikopo makundi maalum yakabidhi ripoti

**Na Julieth Mkireri**

KAMATI maalum iliyoundwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuangalia utaratibu mzuri unaoweza kutumiwa na serikali kutoa mikopo kwa makundi maalum maarufu asilimia 10, imekamilisha kazi yake.

Kamati hiyo ilikabidhi ripoti yake kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMSEMI, Angellah Kairuki jana mjini Kibaha mkoani Pwani.

Ripoti hiyo yenye kurasa 82 ilikabidhiwa katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere iliyoko Kwa Mfipa mjini Kibaha na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Prof. Samweli Wangwe.

Akipokea ripoti hiyo, Waziri Kairuki alimwelekeza Katibu Mkuu- TAMISEMI kukaa na wataalamu katika ofisi hiyo na kuchambua haraka mapendekezo yote yaliyoainishwa katika ripoti hiyo ili kuja na njia moja ambayo ikitumika kutoa mikopo hiyo, itakuwa na tija.

Kamati hiyo iliundwa muda mfupi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza kusitisha utoaji wa mikopo hiyo hadi pale utakapoandaliwa utaratibu mpya wenye tija. Ni baada ya kubainika fedha nyingi hazirejeshwi.

Katika miaka mitano sita ya fedha iliyopita (2016/17-2021/22), jumla ya Sh. bilioni 192 hazijarejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo huku Rais Samia akikiri hazikusanyiki tena kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo kukopeshwa kwa 'watu hewa'.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka jana, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alibaini mabilioni ya shilingi yako hatarini kupotea kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi maalum.

CAG Charles Kichere alibainisha kuwa kwa mwaka huo wa ukaguzi, halmashauri 155 hazikukusanya Sh. bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa makundi hayo.

Kwa mujibu wa CAG, hali iliyobainika katika ukaguzi wake wa mwaka 2020/21 ni mwendelezo wa kile alichokibaini katika miaka mitano iliyopita kuhusu mikopo hiyo.

Katika mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/22 aliyoiwasilisha kwa Rais Samia Machi mwaka huu, CAG Kichere alibainisha kuwa Sh. bilioni 88 zilizokopeshwa na halmashauri kwa makundi maalum kwa mwaka huo wa fedha, hazijakusanywa. Hii ina maana kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi mwaka uliopita wa fedha, jumla ya Sh. bilioni 192 hazijakusanywa kutoka kwa wanufaika wa mikopo hiyo.

**UCHUNGUZI WA CAG**

Katika ripoti yake ya 2020/21, CAG Kichere anabainisha kuwa katika kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya sheria iliyopo, alibaini wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa hawakurejesha Sh. bilioni 47.01 kama marejesho ya mkopo waliopewa.

CAG pia anasema alibaini mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 katika mfuko kama inavyotakiwa kisheria, jambo ambalo linazuia azma ya serikali ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kupunguza umaskini.

"Pia nilibaini mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 178.61 ilitolewa kwa vikundi visivyokuwa na sifa na Sh. bilioni 1.24 hazikuhamishwa kutoka akaunti za amana za mamlaka 11 za serikali za mitaa (halmashauri) kwenda akaunti maalum ya mfuko, kinyume cha Kanuni ya 22(1) na (2) ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu," CAG anabainisha. Anazitaja halmashauri ambazo hazikuhamishia Sh. bilioni 1.24 katika akaunti maalum za mikopo ni: Ushetu (Sh. 308,528,550); Bahi (Sh. 54,222,488); Iringa (Sh. 236,486,588); Busega (Sh. 49,090,000); Nanyumbu (Sh. 179,268,173); Momba (Sh. 41,795,000); Kilolo (Sh. 122,596,622); Gairo (Sh. 38,679,672); Rungwe (Sh. 115,777,111); Ileje (Sh. 32,043,700); na Sengerema (Sh. 59,511,900).

**SHIDA ILIPO**

CAG anabainisha kuwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kunatokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo, akifafanua kuwa mamlaka za serikali za mitaa husika zilitoa mikopo kabla ya kufanya uchambuzi wa kina wa historia ya ulipaji wa kikundi na kupitia mapendekezo ya mradi husika ili kuhakikisha kikundi kina uwezo wa kurejesha mkopo kwa wakati.

Vilevile, CAG anasema amebaini hakuna ufuatiliaji wa karibu wa kukusanya marejesho ya mikopo ambayo bado haijalipwa kutoka kwenye vikundi. Anasema ni dhahiri kuwa kutorejeshwa mikopo kunaweza kuathiri mfuko, hivyo kuufanya usiwe endelevu.

Ili kufikia lengo na uendelevu wa mfuko, CAG anasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo hayajalipwa.

Pia anaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

CAG pia anabainisha kuwa tathmini aliyoifanya katika akaunti za benki za biashara ambako mamlaka za serikali za mitaa hutunza fedha za mfuko, ilibainisha Sh. milioni 156.23 za mfuko zililimbikizwa katika akaunti kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kukopeshwa kwa wanufaika pasipokuwa na sababu za msingi.

Halmashauri zilizokuwa na bakaa ya muda mrefu katika benki za biashara ni za wilaya za Mpwapwa (Sh. 108,703,450) na Nyasa (Sh. 47,530,700).

CAG anataja dosari nyingine katika mikopo hiyo ni kutoshirikishwa kwa wataalamu wa usimamizi wa mikopo katika mchakato wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo.

Anafafanua kuwa Kanuni ya 8 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019, inataka taratibu zote za wa mikopo zisimamiwe na mamlaka za serikali za mitaa.

Pia anaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa mfuko.

"Ninapendekeza kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI itumie benki za serikali au wataalamu wa usimamizi wa dhamana na uwekezaji kama vile Benki ya Maendeleo na Benki ya Biashara Tanzania katika kuongeza ufanisi kwenye kutoa, kufuatilia na kusimamia urejeshwaji wa mikopo na kwa kuzingatia gharama nafuu ya uendeshaji.

"Zaidi ya hayo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inashauriwa kuandaa sera ya mikopo isiyolipika (NPL) ili kusimamia mikopo inayotolewa kwa vikundi husika," CAG anawasilisha hoja yake.

**USULI**

Inaporejewa historia ya mikopo hiyo, inaonyesha kwamba, mwaka 1993 serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambapo wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana.

Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana.

Mnamo mwaka 2019, serikali kupitia Bunge, ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa 2019) kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Kifungu cha 37A(1) cha Sheria hiyo kinazitaka halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa.

# Serikali yaahidi kununua ngano yote ya Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imewahakikishia wakulima mkoani hapa kuwa itanunua ngano yote wanayoizalisha na kuifanya Wilaya ya Makete kuwa kitovu cha uzalishaji wa zao hilo.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa ahadi hiyo jana alipozungumza kwa njia ya simu katika mkutano wa maandalizi ya msimu wa kilimo cha ngano mwaka huu wa fedha.

"Bei ambayo CPB (Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko) itanunua ni Sh. 1,000. Ngano iliyopo sasa hivi itakayovunwa mwaka huu pia watainunua. Makete tutaifanya kama wilaya ya majaribio mwaka huu. Watalima tani 1,000 kwa kuwa mahesabu yanaendelea.

"Tutaifunga Wilaya ya Makete baada ya soil analysis report (ripoti ya uchambuzi wa udongo) kukamilika kuwa ni production area (eneo la uzalishaji) wa ngano peke yake. Ninajua mtaniuliza mahindi tutakula wapi? Tutakapoifunga tutatafuta solution (mwafaka) tutajua mahindi tunakula wapi," alisema Bashe.

Waziri huyo alisema mchakato wa urasimishaji ardhi utakapokamilika, wakulima watakuwa na fursa ya kumiliki ardhi.

"Tutashirikiana nanyi kwenye gharama za kumilikisha ardhi wakulima. Kwa hiyo, eneo lenu litatumika kwa majaribio," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Anthony Sanga, alisema kuwa kupitia mpango wa matumizi ya ardhi, serikali imetoa Sh. milioni 378 kwa ajili ya mchakato huo.

"Kwa hapa Makete, kwa awamu hii, tumepata vijiji 44 kati ya 4,131 nchi nzima ambavyo vinaandaliwa mpango wa matumizi ya ardhi. Tunapoutekeleza na kukamilisha tafsiri yake tunakwenda kupanga maeneo vizuri ya makazi lakini maeneo ya kilimo, malisho, uwekezaji, maeneo rasmi ya vyanzo vya maji, hifadhi za misitu lakini pia kutatua migogoro. Tayari migogoro 16 imetatuliwa hapa Makete," alisema Sanga.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alimweleza Waziri Bashe changamoto ya kukosekana kwa maghala ambayo yatachangia uhifadhi wa mazao kuwa rahisi kwa wakulima.

Mtaka alisema hakuna sababu ya kuwafanya wananchi ya Makete kushindwa kulima ngano badala yake wanapaswa kufanya uamuzi.

Mkurugenzi wa Uzalishaji kutoka Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Jastine Ringo, alisema wametia saini mikataba mitatu ya kuchukua mbegu wilayani humo.

Kaimu Mkurugenzi wa CPB, John Maige, alisema bodi imeanzishwa ili kuhakikisha wakulima wanakuwa na uhakika na mazao wanayozalisha pamoja na kueleza kuwa nchi ina uhitaji mkubwa wa ngano.

Meneja Biashara Kanda ya Nyanda za Juu Benki ya CRDB, Japhary Katura, alisema kwa miaka mitano iliyopita katika kusaidia sekta ya kilimo, wametoa mikopo ya zaidi ya Sh. trilioni 3.6.

Alibainisha kuwa mwezi Januari hadi Machi mwaka huu, imetolewa mikopo ya zaidi ya Sh. trilioni 1.2 katika mazao ya kimkakati.

Mmoja wa mkazi wa mjini Makete, Mexon Sanga, aliiomba serikali kuwawezesha kupata zana za kisasa ili wajikite katika kilimo chenye tija.

## MAKALA

# LENYE NIA NJEMA HALIHITAJI USHABIKI WA WENGI



Na Magabilo Masambu

**Walimu walilazimika kutumia nguvu na viboko zaidi bila wewe kuelewa nia yao njema ambapo tayari leo baada ya kufanikiwa, ndiyo umeweza kuelewa lengo la walimu juu ya maisha yako na kubaki kuwashukuru kwa kusema bila mwalimu fulani leo nisingefika hapa nilipo.**

NCHI nyingi za kiafrika haziendelei kwa sababu nyingi za kiutawala. Moja ya sababu kubwa ni kukosa viongozi bora wenye uamuzi chanya na msimamo katika kutetea na kulinda mali za bara letu.

Sababu nyingine ni kushindwa kuwa na maono ya kitaifa ya muda mrefu na yenye tija katika kujenga uchumi imara.

Pia, kukosa uzalendo wa hali ya juu ambao ndio msingi wa uongozi bora ili kuleta maendeleo ya kweli kwa taifa.

Sifa ya kiongozi bora ni kuwa na maono, aone njia ya kutatua matatizo makubwa na yaliyoshindikana kwa wananchi wake.

Hivyo kiongozi wa namna hii, hasubiri maoni ya wengi juu ya jambo ambalo anaona ni muhimu kwa watu wake, mradi liwe jema kwa nchi, hivyo kujitosa na wachache walioweza kuelewa umuhimu wa jambo lenyewe ambapo baadaye, wengi huelewa umuhimu wake baada ya lengo kutimia kama lilivyokusudiwa na kuonekana kwa watu wote kuwa lina maslahi kwa Taifa.

Sifa kubwa ya kiongozi ni kuona njia, wanaoongozwa wengi huwa hawaoni njia, hivyo akiwauliza juu ya anachokiona yeye, wengi hawaoni kitu. Inawezekana ikawa ngumu sana watu hao kuamini kiongozi anachokiona na hivyo kushindwa kufikia lengo.

Kulingana na ukweli huo, kiongozi bora huamua kufanya mambo ya msingi bila kujali wangapi wataelewa umuhimu wa shughuli anayoiamua bali hutambua fika kuwa wengi watamwelewa baada ya matokeo.

Watu wengi duniani hutaka wanavyoviona au wanayoyaona kupitia macho yao, wachache huona wanayoyataka akilini katika fikra zao. Hivyo, watu hawa ndiyo wameleta teknolojia, mabadiliko makubwa ya kisayansi na mambo mengi mbalimbali muhimu yote yaonekanayo leo kwa macho katika ulimwengu.

Mfano, aliyeunda gari aliona alichokitaka katika akili na fikra zake na aliiona picha ya gari akilini likitembea barabarani na kwamba siku moja litumiwe na watu wote na kama angelichukua hatua ya kuwaomba maoni juu ya kile alichokiona akilini, hakika gari lisingewezekana, wengi wangelisema 'unachowaza hakitawezekana', hivyo gari lingebakia kichwani mwa yule aliyewaza.

Lakini aliyenunua lile gari alipenda alichokiona kwa macho yake.

Hebu fikiria ushawahi kujiuliza kwanini uliwahi kuwachukia walimu wako darasani kila walipokuadhibu umekosea na kuwaona kama maadui zako? Jibu ni kwamba, uliwachukia kwa sababu hukujua kuwa walikutakia mema zaidi katika kukuandaa kimaisha na kuishi vizuri.

Walimu walilazimika kutumia nguvu na viboko zaidi bila wewe kuelewa nia yao njema ambapo tayari leo baada ya kufanikiwa, ndiyo umeweza kuelewa lengo la walimu juu ya maisha yako na kubaki kuwashukuru kwa kusema bila mwalimu fulani leo nisingefika hapa nilipo.

Viongozi wanapaswa kwanza wawe na uwezo mkubwa katika kupambanua faida na hasara ya mambo katika nchi.

Ni hali itakayowafanya waanze kuelewa mambo muhimu ya kimaendeleo ambayo wana wajibu wa kuyafanya bila wengine kuelewa kusudi, bali kusudi litaonekana baada ya kufanyika mambo hayo na kuleta maendeleo kwa wananchi wote yanayoonekana.

Watu makini huona fursa ya mwanga katikati ya giza nene, wakati huo wengine huona kero katikati ya giza nene. Kwa maana hiyo, watu wengi hawaamini kuwa inawezekana na hivyo ukiwasikiliza ushauri wao mara nyingi hupoteza.

Israel iliona fursa katikati ya ukame mkubwa na jangwa lililoenea nchi nzima, wakachimba visima virefu na kuwekeza katika kilimo cha matunda. Leo wao ni nchi inayosambaza matunda duniani kote. Lakini uamuzi huo ulifanywa na viongozi makini tu wenye maono yenye tija kwa taifa.

Kinyume cha haya yote itakuwa ni bahati mbaya kama tutapata viongozi ambao watakuwa na maono ya kuyaingiza mataifa yetu haya katika matatizo kwa manufaa yao binafsi ya muda mfupi.

Kelele nyingi za waafrika juu ya viongozi wao, zimekuwa zikiashiria kwamba wapo baadhi ya viongozi ambao wanawaza kwa niaba ya wananchi lakini wakikusudia kujinufaisha binafsi na kila atakayekuja huko mbele 'atajijua mwenyewe'.

Ushauri wangu kwa viongozi wetu wote, tuwe na maono kwa manufaa ya watu tunaowaongoza.

Ni muhimu kuhakikisha yote kwa pamoja yalenge kulijenga taifa.

Lakini viongozi mnayo nafasi zaidi ya kutazama ni mambo gani yatakayowafaa wananchi na mataifa yetu kwa ujumla, tumewapeni dhamana ya kuongoza kwa niaba yetu siyo badala yetu na hivyo tunategemea uamuzi wenu uwe na nia njema kabisa na mataifa yetu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Kumekucha,' wimbo 'tata' wa Marijani, viboko shuleni



Na Adam Fungamwango

**Kulingana na ukweli huo, kiongozi bora huamua kufanya mambo ya msingi bila kujali wangapi wataelewa umuhimu wa shughuli anayoiamua bali hutambua fika kuwa wengi watamwelewa baada ya matokeo.**

KUMEKUCHA sasa kumekucha, majogoo vijijini wanawika, hata na jua mbinguni linatoka, wazalendo amkeni tufanye kazi sasa..."

Huu ni wimbo maarufu sana kuanzia katikati ya miaka ya 1970, hadi katikati ya miaka ya 1990.

Na umaarufu wake hasa ulikuwa ni kwa wanafunzi wa wakati huo. Hakuna mwanafunzi yeyote wa miaka hiyo ambaye haufahamu wimbo huu.

Ni wimbo uliopigwa na bendi ya Safari Trippers, ulitungwa na marehemu jabali la muziki, Marijani Rajabu.

Sidhani kama kuna mwanafunzi yeyote wakati huo aliyekuwa anajua wimbo huu umepigwa na bendi gani au mtunzi. Hakuna aliyetaka kujua hilo.

Ni kwa sababu wengi walikuwa hawaupendi. Siyo kwamba ulikuwa wimbo mbaya, ulipigwa vibaya, au mwimbaji wake hakuwa mahiri kwenye uimbaji, la hasha.

Huu ni wimbo ambao ulikuwa ukipigwa redioni majira ya kuanzia saa 11:30 hivi na ndiyo uliokuwa ukitambulisha muda kuwa sasa ni wakati wa kuamka na kwenda shule.

Ulipigwa kuashiria kuanza kwa kipindi kilichokuwa kinaitwa 'Kumekucha', ambacho kilichukiwa tu na wanafunzi kwa sababu kiliwekwa muda ambao walikuwa wanatakiwa waamke kwenda shule.

Mwanafunzi yeyote yule wakati huo akiusikia wimbo huo kama amelala, basi tayari kwake ni ishara kuwa aamke mara moja na kufanya maandalizi ya kwenda shule, jambo ambalo kwa wanafunzi wengi ambao ilikuwa shida kwani ni wakati ambao usingizi unakuwa mtamu sana.

Kwa wafanyakazi, yaani waliokuwa watu wazima wakati huo, kwao wala haikuwa shida, lakini shughuli ilikuwa kwa wanafunzi, kwani utoto bado ulikuwa unasumbua.

Kuamka alfajiri hadi kwa wanafunzi wa leo, ni tatizo kubwa. Mara nyingi wazazi hutumia mbinu mbalimbali za upole na ukali kuwaamsha watoto wao ili waende shule.

Burudani inakuja kipindi cha baridi kali, au siku za mawingu au mvua, halafu denti kajifunika shuka gubigubi, masikio yake yanakutana na wimbo huo.

Ikumbukwe zamani redio ilikuwa ni moja tu, Redio Tanzania, hivyo haikuwa rahisi kukwepa kuusikia. Hata kama mzazi hakuwa na redio, lakini unaweza ukausikia hata kwenye nyumba ya jirani.

Ni wakati ambao mwanafunzi anatakiwa aamke haraka ajiandae na kwenda shule kuwahi namba. Kumbuka kama hukupata namba, unahesabika kuwa umechelewa.

Na mara nyingi wakati huo zilihesabiwa saa 12:00 asubuhi.

Sasa unaweza kuusikia wimbo huo, ukaamka kwa kujivutavuta mwenyewe au ukaamshwa kwa nguvu na mlezi au mzazi, ukajiandaa na kuondoka nyumbani.

Lakini inategemea pia umbali wa nyumbani na shule pia. Njiani unaweza kuusikia tena wimbo huo huo ukiimbwa.

*"Sasa kaziii, oooo mama, ooo mama ooo, sasa kaziii, acha mchezo na kazi, ooo mama..."*

Ukisikia hivyo kwenye redio kama uko njiani kwenda shule, ujue umechelewa namba. Sasa ni hiari yako, uharakishe uende ubahatishe labda siku hiyo wamechelewa kidogo kuhesabu namba, au uamue kutembea taratibu kwa sababu hakuna faida tena ya kuharakisha, na bakora za uchelewaji zitakuwa zinakusubiri.

Ni kwamba ukisikia kipande hicho, ni kwamba kipindi cha 'Kumekucha' ndiyo kinamalizika. Na inakuwa ni saa 12:00 za asubuhi. Ni muda ambao mwanafunzi alitakuwa awe ameshafika shuleni.

Hii ndiyo sababu kubwa iliyosababisha kipindi hicho cha 'Kumekucha' kichukiwe mno na wanafunzi wengi wakati huo kutokana na kuwekwa kwenye wakati ambao kunakuwa na mchakato wa wao kuamka na kwenda shule.

Ukiachana na kipindi hicho, kipindi kingine ambacho hakikuwa rafiki kwa wanafunzi, bali watu wazima ni 'Mashairi'.

Mghani maarufu wa wakati huo ni Athumani Khalfan. Ni kipindi kilichopendwa na watu wengi, hasa watu wazima.

Wanafunzi wengi walikuwa hawakipendi kwa sababu nacho kilipata bahati mbaya ya kuwekwa mida ya saa saba hadi nane, kipindi ambapo zamani ndiyo muda wa wanafunzi kurudi majumbani.

Ni kipindi ambacho wanafunzi wengi wanarejea wakiwa na njaa, hivyo njiani wakisikia mzee huyo akighani mashairi, wao akili yao iko kufika nyumbani upesi ili wapate chakula.

Kwa bahati mbaya sana unaweza kurejea nyumbani ukakuta siku hiyo yamepikwa maharage yasiyoiva upesi hadi yatiwe magadi, na ukiendelea kusikia mashairi yale, unatamani kulia.

Ndiyo maana hadi leo wakiwa watu wazima, wakisikia ghani ile ya mashairi kila mmoja anachokumbuka ni njaa ilivyokuwa inamuuma akirejea kutoka shule, au akifika nyumbani na kukuta chakula kimechelewa.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa ni kwamba hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.
Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-17

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Pendo alisimama na kwa sababu hakuwa amekaa mbali sana, alisogea hatua kama sita kwenda pembeni, akakutana na Husna. Wakakumbatiana, wahudhuriaji wakazidi kushangilia.

"Pole mwenzangu kwa yaliyokukuta." Pendo alimnong'oneza.

"Ahsante sana."

"Ndiyo ukubwa mwenzangu, ndoa zina changamoto, si unaona, hayo yaliyokukuta ndiyo yamenikuta mimi. Hiyo simu uliyopigiwa ilikuwa ya kwangu. Kilichokukuta ndiyo hicho hicho kilichonikuta, na mimi pia nilikuwa nimeolewa muda si mrefu na mume wangu pia alikuwa hayupo, ndiyo maana kila kilichozungumzwa kilikuwa kinakugusa moja kwa moja."

"Mwenzangu, mbona makubwa." Husna akajibu huku kila mmoja akimpa mwenzake simu yake. Simu zilizobadilishwa kwa fundi simu na kuzua tafrani kwenye ndoa ya Dan.

Belo alinyanyuka akionekana ana jambo.

"Naomba pia, Zawadi uende kwa wenzako pale, nawe upate picha ya pamoja na wenzako."

Zawadi naye alinyanyuka na kuwafuata Husna na Pendo.

"Husna, huyu ndiye aliyekuwa mgomvi wangu, na ndiye aliyekupigia wewe akidhani ni mimi. Mimi nimemsamehe kwa yote juu ya mume wangu na sasa hivi tupo pamoja, ni shoga yangu hatari, naomba na wewe umsamehe."

"Pendo mimi nimemsamehe kwa sababu kumbe alikuwa anadhani anaongea na mtu mwingine."

"Nisameheni wote wawili, waswahili wanasema wagombanao ndiyo wapatanao." Zawadi aliomba msamaha huku akiwakumbatia wote wawili. Wapigapicha za mnato na video walikuwa wanachukua kumbukumbu. Wenye simu janja nao hawakuwa nyuma. Kila mtu alikuwa anarekodi anavyojua yeye.

"Na kama mmenisamehe shoga zangu, mwezi ujao nafunga ndoa nawakaribisha wote wawili mje, yaani mkija nitafurahi mimi, na nitaona kweli mmenisamehe ili tujenge urafiki na undugu." Zawadi aliomba.

"We lete sare bibi, mimi ndiyo shughuli zangu hizo, nitazoa shoga zangu kutoka Mabibo na Mburahati, hutoamini." Wote waliangua vicheko kwa furaha kama vile wanafahamiana muda mrefu kiasi cha kuwashangaza wote mle ndani.

"Siku hiyo nitacheza kama mama yake mwali." Pendo alidakia na kuwafanya wafurahi zaidi.




**"Nilikuwa sijamaliza upande wa mume wangu. Kwa yote niliyoyasikia hapa na yaliyojidhihirisha, sina haja hata ya kumsamehe." Maneno haya yalifuatiwa na mshtuko, ukiambatana na mshangao mkubwa kutoka kwa watu wote.**

Furaha yao watu watatu iliwafanya watu mle ndani nao kuzidisha furaha. Belo na Massawe nao walikuwa kwenye kilele cha furaha, kwani walichokibuni na kukifanyia kazi kimeleta matokeo chanya. Walicheka na kukumbatiana.

Zilipita kama dakika tano za furaha, kabla ya watu kurejea kwenye hali ya kwaida, ingawa walionekana kuchangamka zaidi.

Kila mtu alisahau kama muda ule wote ulikuwa ni karibu ya kuahirisha sherehe hiyo. Matokeo yake ilionekana kama vile ndiyo kwanza inaanza.

Awali watu walionekana kukaa kwa umakini sana, kila mmoja akiongea na mwenzake kikawada sana. Lakini kwa muda huu ambao kila mtu alikuwa 'ametapika nyongo' na mambo yote kujulikana, watu walionekana kama wamezoeana, hivyo zilianza stori zingine kabisa tofauti na zile za mwanzo.

"Jamani ngoja nihitimishe basi." Husna aliwashtua watu ukumbini. Walipunguza sauti na kila mmoja sasa alikaa sehemu yake. Shoga zake walikaa pembeni yake. Ni kwamba waliokaa kwenye viti vya kulia na kushoto kwa Husna alitoka na kuwapisha zawadi na Pendo ili kuwafanya waendelee kujenga urafiki yao.

Vinywaji vililetwa tena, ikawa kama vile pati inataka kuanza upya kabisa. Hakuna mtu aliyekumbuka nyumbani kabisa.

"Nilikuwa sijamaliza upande wa mume wangu. Kwa yote niliyoyasikia hapa na yaliyojidhihirisha, sina haja hata ya kumsamehe." Maneno haya yalifuatiwa na mshtuko, ukiambatana na mshangao mkubwa kutoka kwa watu wote.

"Kila kitu kimejidhihirisha kwa watu, sasa kwanini hataki kusamehe?" Wakajiuliza.

"Binadamu husamehewa kama amefanya makosa, au mtu humsamehe mwenzake kwa kufanyiwa makosa au kukwazwa, lakini hapa naona kama vile mume wangu hajafanya kosa lolote..." Hapo ndipo watu walipoelewa Husna alikuwa anataka kusema nini, au anamaanisha kitu gani. Likazuka shangwe, miluzi na vigelegele ukumbini hapo.

"Mume wangu Dan hajui lolote masikini ya Mungu, hajanikwaza, nimsamehe ya nini? Ni kwamba kilichotokea hapa kila mtu anakifahamu. Tena afadhali mimi nimekuwa mmoja wa walipitiwa na sakata hili kwa kusikia simu ya mwanamke. Lakini yeye tangu mwanzo hadi mwisho hajui lolote hadi amekuja kujua leo hii. Nilipoondoka kwenda kwetu najua alisononeka sana akiwa hajui kitu gani kimetokea. Alifanya kila njia hadi kunifuata kunibembeleza, lakini kilichotokea, sitaki kusema kitu chochote. Mimi ndiyo namuomba radhi ya kile kilichotokea alipokuja nyumbani. Mume wangu nakuomba njoo."

Dan haraka alifika kwa mkewe. Husna alimpokea kwa kumkumbatia mumewe na kumuomba msamaha.

"Hata mimi kilichoongelea hapa kusema kweli imekuwa 'sapraizi', sina cha kuongeza, namshukuru sana kama Belo na Massawe na kufanya hafla hii ya kukumbukwa kwenye maisha yetu yote ya ndoa yaliyobaki. Nakupenda mke wangu, nakuomba rudi nyumbani."

"Leo hii hii tukitoka hapa, tunaondoka wote." Jibu hilo la Husna niliibua ukumbi kwa vigelegele, shangwe na nderemo kama vile ilikuwa ni siku ya harusi.

Pendo na Zawadi walisimama, na kuhanikiza kwa vifijo na kuufanya watu wote ukumbini kujawa na furaha isiyomithilika. Wakaanza kuimba na kupiga makofi. Dan na mkewe Husna walikuwa wamekumbatiana kwa mara ya kwanza baada ya miezi mitatu ya sintofahamu, mashaka, tabu, misukosuko, fadhaha na kukatishwa tamaa.

"Dj weka ngoma." Sauti ya mtu mmoja ilisikika.

"Liwalo na liwe, leo namtangaza, sitaki nishauriwe, eee namtangaza, huyu hapa huyu, nampenda, ananipenda..." wimbo wa Mbosso uliowekwa na Dj, 'Huyu Hapa', ulirindima, akisababisha watu wengi waache viti na kuanza kuserebuka. Dan na Husna walicheza wakiwa wamekumbatiana. Pendo na Zawadi walicheza kando yao wakiwapepea na vitambaa vyao.

Ilionekana kama sherehe ndiyo kwanza zimeanza upya. Hakuna aliyekumbuka tena kuondoka. Hata aliyekuwa anataka kufunga pati hiyo alisahau.

Watu wawili Belo na Massawe walionekana wamesimama tu bila kucheza, waliwashangaa wenzao ukumbini. Furaha iliwazidi, wakashindwa kufanya chochote. Wakabaki wamesimama kwa mshangao. Ni kama hawaamini wanachokiona.



# DIAMOND PLATNUMZ ACHAFUKWA

STAA wa Bongo fleva Naseeb Abdul, Diamond Platnumz, amechafukwa, kwenye page yake ya insta stori ameposti meseji zinazoonyesha anakerwa na watu wanaomsemasema, kumteta na kuona kama ameishiwa.

Lakini kwenye ujumbe wake huo ametoa 'vitisho' kuwa sasa wasanii wote wakae chonjo, mzee wa kazi anaingia mwenyewe mtamboni.

Inaonekana tayari ana ngoma mpya kibao ambazo ataziachia mfululizo na hatoacha jiwe juu ya jiwe lingine.

Meseji yake hiyo ndefu imeshtua wengi na kuwafanya mashabiki wake na muziki wa bongo fleva sasa wamekaa mkao wa kula ili kuona nini kitatokea hivi karibuni. Wasanii nao baada ya kupigwa mkwara, wamekaa kuangalia ni kitu gani anachotaka kukifanya mkali huyo wa muziki wa kizazi kipya ndani na nje ya nchi.

Diamond ameandika maneno yafuatayo.

"Wakati naanza harakati za kutoka nje ya Afrika Mashariki wengi mlichelewa kunielewa na mkaanza kusema 'ooh nimeishiwa utunzi, ooh naimba ujinga', na kashfa kibao.

Mkaanza kuwapa vichwa wasanii wasio levo yangu washindane nami, kuja kuhstuka nawaletea matuzo ya kimataifa na kujaza viwanja kimataifa ambayo mlizoea kuyasoma kwenye Jiografia, huku wasanii wetu wakiwa wanasubiri matamasha ya redio.

Hivyo kama mlivyokaa kwa kutulia wakati natega mabomu yangu ya nje ya Afrika Mashariki, naomba mkae kwa kutulia vivyo hivyo ninapoanza mashambulizi yangu, sitaki maoni wala ushauri. Ushauri pelekeni angaza.

Kama washauri wazuri, wakati nilipokuwa kimya nikidili na media, mngewashauri hao wasanii wenu mnaowashindanisha ili wafanye hata robo ya nilichokuwa ninakifanya kwenye matuzo, majukwaa, kupunguza hizi dharau za Wanigeria, lakini vyote viliwashinda. Wanaume tunayaweza kunapoanza, tunaomba mtulie.

Julai ni mwezi wa kuzaliwa kwa mama yangu, na kuanzia mwezi huo itaanza rasmi mvua ya mawe. Zangu zitakuwa ni kolabo za nje na ndani," alisema Diamond na hakuishia hapo akaendelea.

"Na nitahudumu hapo kwa namba moja kuanzia Julai 2023 hadi Januari 2024, nitampisha msanii wangu mpya WCB na ninaheshimiana nao.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SILVA ATAKIWA PSG**
LUIS Enrique anamtaka winga wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28, atakapochukua nafasi ya Christophe Galtier kama kocha mpya wa Paris St-Germain . **(90min)**

**FELIX NAE AWINDWA**
PIA Luis Enrique ambaye ni kocha wa zamani wa Hispania anataka PSG kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 23 kutoka Atletico Madrid. **(Relevo)**

**TAREMI AWANIWA MAN**
KLABU ya Manchester United inamlenga mshambuliaji wa FC Porto na Iran, Mehdi Taremi mwenye umri wa miaka 0. **(Jornal de Noticias)**

**LUKAKU NA CHELSEA**
CHELSEA inakaribia kufikia makubaliano na Inter Milan kuhusu uhamisho wa kudumu wa mshambuliaji wao wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30. **(90min)**

**AZPILICUETA ARUHUSIWA**
CHELSEA imekubali kumruhusu mlinzi wa Hispania, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 33 kujiunga na Atletico Madrid kwa uhamisho wa bila malipo. **(Marca)**

**ARSENAL NA RICE**
KLABU ya West Ham ina matumaini ya kukubaliana na Arsenal kuhusu malipo ya pauni milioni 105 kwa kiungo wao wa kati, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, kufikia Jumatatu. **(Sun)**

**FRED ATAKIWA ROMA**
KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho anataka kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Fred mwenye umri wa miaka 30 kutoka klabu yake ya zamani ya Manchester United . **(Sun)**

**PULISIC HUYO MILAN**
CHRISTIAN Pulisic wa Chelsea amekubaliana kimsingi kuhusu mkataba wa muda mrefu wa kujiunga na AC Milan, lakini klabu hizo bado hazijakubaliana kuhusu ada ya uhamisho wa winga huyo wa Marekani mwenye umri wa miaka 24. **(ESPN)**

**ZIYECH BASI TENA**
PENDEKEZO la Hakim Ziyech kuhama kutoka Chelsea kwenda Al Nassr limezimwa baada ya winga huyo wa Morocco mwenye umri wa miaka 30 kushindwa kufikia vigezo katika vipimo vya afya. **(Mail)**

**CHELSEA NA CAICEDO**
CHELSEA itaongeza juhudi zao za kumsajili kiungo wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21 na wanatumaini kuwa ada ya takriban pauni milioni 80 inaweza kuafikiwa na Brighton. **(Standard)**

**MAN KUUZA KWANZA**
KLABU ya Manchester United italazimika kuuza kabla ya kumnunua mlinda mlango wa Inter Milan raia wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27. **(Talksport)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# PULISIC AKUBALI KUJIUNGA NA MILAN

●●●Kiungo huyo amekubali kupunguza mshahara wake ili kukamilisha usajili huo na kuhamia Italia..

**MILAN, Italia**

MCHEZAJI wa kimataifa wa Marekani, Christian Pulisic ana makubaliano ya kimsingi juu ya mkataba wa muda mrefu wa kuondoka Chelsea na kwenda kwa wababe wa Serie A, AC Milan, ingawa klabu hizo bado hazijakubaliana juu ya ada ya uhamisho, kwa mujibu wa ESPN.

Pulisic mwenye umri wa miaka 24 yuko tayari kuchukua punguzo kubwa la malipo ya mshahara wake ili kufanya uhamisho huo ufanyike.

Mazungumzo yamesalia juu ya ada ya uhamisho, huku Chelsea ikitaka euro milioni 25 na Milan ikifikiria kutoa kati ya euro milioni 15 hadi 18.

Habari hiyo iliripotiwa kwa mara ya kwanza na kituo cha Italia cha Tuttomercatoweb.

Chelsea inaamini kwamba kuhama kwa Sandro Tonali kwenda Newcastle United kunamaanisha kuwa Milan wanaweza kumudu kulipa zaidi, lakini Milan wanataka mapato kutoka kwa mpango huo kuwasaidia kupata wachezaji watatu hadi wanne.

Pulisic mwenyewe ameshaweka wazi kwamba anataka tu kwenda Milan. Pulisic, aliyesajiliwa kwa euro milioni 64 kutoka Borussia Dortmund mwaka 2019, amebakiza miezi 12 katika mkataba wake na Chelsea.

Huku klabu hiyo ikihitaji kupunguza ukubwa wa kikosi chao na bili ya mshahara baada ya kutumia zaidi ya pauni milioni 600 kununua wachezaji wapya tangu klabu hiyo iliponunuliwa na Pulisic yuko juu kwenye orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kuondoka.

Klabu nyingi zimefuatiliwa kuhusu uwezekano wa kumsajili Pulisic, huku vyanzo vya habari viliiambia ESPN hapo awali kwamba Manchester United, Newcastle, Napoli, AC Milan na Galatasaray zote zilionesha nia ya kumuwania.

Pulisic amekumbana na majeraha akiwa Chelsea katika misimu miwili iliyopita. Alizomewa na sehemu ndogo ya wafuasi wa klabu hiyo alipotambulishwa kama mchezaji wa akiba kipindi cha pili wakati wa mchezo wa mwisho wa msimu uliopita wakiwa nyumbani dhidi ya Newcastle.

HABARI MICHEZO

# MAN UNITED KUMPA MKATABA MPYA DE GEA




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inapanga mazungumzo ya ana kwa ana na David de Gea katika jitihada za kumbakiza golikipa huyo ambaye mkataba wake umemalizika, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mkataba wa De Gea Old Trafford ulimalizika juzi Ijumaa na sasa mlinda mlango huyo ni mchezaji huru.

Anaoa wikendi hii na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United imemruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 32 kutumia wakati wake na familia yake nchini Hispania.

Hata hivyo, mabosi wa klabu akiwemo mkurugenzi wa soka, John Murtough wana nia ya kukutana na De Gea ana kwa ana ili kujadili hali ya mkataba wake.

Katika taarifa baadaye siku ya Ijumaa, United ilisema kwamba, mkataba wa David De Gea unakaribia kumalizika, lakini majadiliano yanabaki wazi na kipa huyo aliyekaa muda mrefu.

Kocha Erik ten Hag amesema hadharani anataka Mhispania huyo abaki, ingawa klabu hiyo imekuwa na nia ya kupunguza mshahara wake wa kila wiki wa karibu pauni 375,000 kwa wiki.

United walikuwa na chaguo la kuongeza mkataba wa De Gea kwa mwaka mmoja hadi 2024, lakini waliamua kutoanzisha kipengele hicho.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba United pia inazungumza na wawakilishi wa Andre Onana kwa nia ya kutoa ofa kwa kipa huyo wa Inter Milan.

Ten Hag anamfahamu vyema mchezaji huyo wa kimataifa wa Cameroon baada ya kukaa pamoja Ajax.

Pia kuna nia ya kuwanunua Diogo Costa wa FC Porto na David Raya wa Brentford.

United wameongeza mkataba wa Tom Heaton kwa mwaka mwingine na Dean Henderson amerejea katika klabu hiyo baada ya kukaa kwa mkopo msimu uliopita kule Nottingham Forest.

## Atletico Madrid yaipiku Inter kwa Azpilicueta

**MADRID, Hispania**

ATLETICO Madrid imetoa ofa ya saa 11 kwa mlinzi wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, kwa mujibu wa 90minutes, huku Los Rojiblancos hao wakipania kuwapiku Inter kwenye kuwania saini ya beki huyo.

Azpilicueta alikubalina maslahi binafsi na Inter mapema mwezi huu na alitarajiwa kuelekea Italia kwa uhamisho wa bure.

Hata hivyo, Atletico wamejipanga kwenye mazungumzo na ofa ya kumrudisha Azpilicueta katika nchi yake ya Hispania.

Kurejea Hispania kunafahamika kuwa kutavutia zaidi kwa Azpilicueta na familia yake na hivyo Atletico sasa wanatarajiwa kuinasa saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33.

Atletico wamemwachia beki wa kulia wa zamani wa Tottenham Hotspur, Matt Doherty msimu huu wa joto na hivyo kuna nafasi wazi katika safu ya ulinzi ya Diego Simeone ambayo Azpilicueta ataijaza.

Azpilicueta sasa anahitaji kukamilisha maelezo ya kuondoka kwake Chelsea.

Beki huyo mkongwe bado amebakiza miezi 12 katika mkataba wake pale Stamford Bridge, lakini makubaliano ya kuachanana msimu huu hayatarajiwi kuwa na matatizo.

Chelsea iko tayari kwa kuondoka kwa Azpilicueta, na ilifikia makubaliano Januari kumsajili Malo Gusto mwenye umri wa miaka 20 kutoka Lyon kwa ada ya pauni milioni 30.



# Barcelona yamtema Umtiti

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imefikia makubaliano na Samuel Umtiti kumwacha beki huyo licha ya kubakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake.

Umtiti mwenye umri wa miaka 29 anapatikana kama mchezaji huru msimu huu wa joto baada ya kutumia msimu uliopita kwa mkopo katika klabu ya Lecce ya Italia.

"Barcelona na Umtiti wamefikia makubaliano ya kusitisha mkataba," ilisema taarifa ya Barcelona jana.

"Klabu inapenda kutoa shukurani zake kwa Umtiti na inamtakia kila la kheri na mafanikio katika siku zijazo."

Umtiti alijiunga na Barca kutoka Lyon mwaka 2016 kwa euro milioni 25 na alijiimarisha kama mchezaji wa kikosi cha kwanza pamoja na Gerard Pique katikati ya safu ya ulinzi, akichukua nafasi ya Javier Mascherano.

Kiwango hicho kilisababisha mkataba mpya na nyongeza ya mshahara mwaka 2018 lakini mfululizo wa majeraha ya goti baada ya kushinda Kombe la Dunia mwaka huo akiwa na Ufaransa yaliathiri kiwango chake.



Baada ya kucheza mechi 83 katika misimu yake miwili ya kwanza akiwa na Barca, alicheza mechi 50 tu katika misimu minne iliyofuata kabla ya kukubali kujiunga na Lecce ya Serie A ili kuanza maisha yake ya soka msimu uliopita.

Kabla ya hapo alikuwa amekubali kuongeza mkataba na Barca ili kupambania nafasi yake.

Nchini Italia msimu huu uliopita alicheza mechi 25 na kumsaidia Lecce kusalia Serie A.

Hata hivyo, kiwango chake hakijamrudisha kwenye mipango ya Barca, huku Ronald Araújo, Andreas Christensen, Jules Koundé na Eric García wakiwania nafasi ya beki wa kati.

HABARI MICHEZO

# AZAM KUANZA KAMBI JULAI 9 TUNISIA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Azam imekuwa klabu ya kwanza kutangaza tarehe rasmi ya kuanza maandalizi ya msimu ujao wa mshindano, huku ikitarajia kupiga kambi yake nchini Tunisia kuanzia Julai 9.

Klabu ya Singida Fountain Gate ambayo nayo itacheza Kombe la Shirikisho barani Afrika pia ilitangaza kuwa itapiga kambi nchini humo lakini haikutaja tarehe rasmi.

Msemaji wa Azam FC, Hasheem Ibwe amesema jana kuwa kikosi cha wachezaji wote wa Azam kitaondoka nchini Julai 9 kwenda Tunisia kuweka kambi hadi Julai 30 kujiandaa na Ligi kuu na mashindano ya kimtaifa ya CAF .

"Tunataka kuingia kambini mapema kwa mapendekezo ya Kocha wetu Youssouph Dabo ambaye anataka kuangalia kile alichokuwa akiangalia kwenye mechi za mwisho msimu uliomalizika ili ligi ikianze tuianze vizuri na kufikia malengo yetu," alisema Ibwe na kuongezea,

Mpaka kufikia tarehe 3 wote wanatakiwa kuripoti klabuni kwa ajili ya vipimo, kuangalia utimamu wa mwili, kuanzia tarehe 4 rasmi mazoezi yanaanza na tarehe tisa Mungu akipenda timu itaondoka kuelekea Tunisia kwa ajili ya 'pre season' , " alisema Ibwe.

Aidha, alisema kikosi ca timu kinatarajia kurejea nchini Julai 30 kwa ajili ya tamasha la klabu hiyo la Azamka wanalotarajia kufanya tarejea Julai 30 mwanzoni mwa mwezi wa nane.

Kuhusu usajili, Ibwe alisema kwa sasa wamebakiza kuwatambulisha wachezaji wawili tu wa kigeni ili kuufunga msimu usajili msimu huu.

"Awali tulidhani tunaweza kusajili wachezaji wasiopungua saba kwa ajili ya msimu ujao, lakini kwa yeye mwalimu alivyotaka na kuwaona wachezaji wetu, anataka wachezaji watatu tu wa kigeni ambao ni wapya kabisa na mchezaji mmoja mzawa ambaye ni Feisal Salum, kwa hiyo hapo wamebaki wachezaji wawili tu, tutawatambulisha muda wowote kuanzia sasa" alisema Ibwe.

Wakati huo mchezaji mpya wa timu hiyo raia wa Gambia, Jibril Sillah, anatarajia kutua leo baada ya kushindikana kufanya hivyo Ijumaa iliyopita.

Ibwe alisema mchezaji huyo aliyekuwa mchezaji wa Raja Athletic Club ya Casablanca Morocco, lakini akiichezea Jeunesse Sportive ya nchini humo kwa mkopo atawasili na kwenda moja kwa moja kwenye ofisi za klabu hiyo Mzizima kwa ajili ya kukamilisha taratibu zote za usajili.

"Ni kweli tulitoa taarifa angewasili Ijumaa, lakini kutokana na majukumu yake kwenye timu ya taifa ya Vijana ya Gambia, sasa tunamtegemea kuwasili Jumapili (leo) jioni, atawasili kwa ajili ya kumamilisha taratibu za mwisho za kujiunga na timu yetu," alisema Ibwe.




Mkurugenzi wa MultiChoice Talent Factory Africa, Nwabisa Matyumza (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu mafunzo ya waandishi wanaoandaa filamu visiwani Zanzibar. Kulia ni Mkurungenzi wa Jukwaa la ZIFF, Martin Muhando na Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Dk. Kiango Kilonzo. Kushoto ni Victoria Golo na Neil Mecarthy ambao ni wakufunzi wa uzalishaji wa filamu . PICHA: MPIGA **PICHA WETU.**

# Kidunda akiri Mukadi mgumu

Na Saada Akida

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Seleman Kidunda amesema pambano lake la juzi dhidi ya Erick Mukadi kutoka Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo lilikuwa gumu kutokana na ubora wa mpinzani wake huyo.

Kidunda alisema licha ya kushinda kwa pointi, Mukadi alionyesha ugumu kwenye raundi zote za pambano hilo.

"Halikuwa pambano jepesi, jamaa ni mgumu sana, lakini nashukuru kuweza kushinda pambano hili," alisema Kidunda muda mfupi baada ya kumalizika kwa pambano hilo usiku wa kuamkia jana.

Katika pambano hilo la raundi 10 lilifanyika kwenye ukumbi wa Mlimani City Jijini Dar es Salaam, Kidunda alifanikiwa kumuangusha mara nne mpinzani wake huku akionyesha uwezo mkubwa uliopelekea kushangiliwa na mashabiki wengi waliokuwepo ukumbini hapo.

Kidunda alifanikiwa kumuangusha mara mbili Mukadi katika raundi ya kwanza kabla ya kumuangusha tena kwenye raundi ya tisa lakini hiyo haikupelekea kumchapa kwa KO mpinzani wake ambaye alionekana kuzidi kuimarika katika kila raundi kwa kadri muda ulivyokuwa unaenda.

Kidunda ambaye ni Askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), mara baada ya pambano hilo aliwashukuru wadau wote waliojitokeza kwenye Ukumbi huo akisema kwa sasa yupo tayari kuletewa bondia yoyote kutokana na kurudisha kiwango chake.

"Binafsi nashukuru Mungu kwamba kila jambo limeenda vizuri kuelekea katika pambano hili, nimefanikiwa kushinda kwa ushindi mkubwa kila mmoja aliyefika ameweza kuona ngumi biriani na amefurahi kwa nilichoweza kukifanya japo nilipata upinzanimkubwa kutoka kwa Mukadi, kwa sasa nipo tayari kupambana na bondia yoyte wa uzitowangu," alisema Kidunda.

Katika pambano lingine bondia Mfaume Mfaume alifanikiwa kumchapa kwa pointi Chikondi Makawa wa Malawi, pia Pius Mpenda alishinda kwa pointi dhidi ya Simon Tcheta kutoka Malawi katika mapambano ya utangulizi yaliopigwa kwa raundi nane.

## Simba yaanza mazungumzo

INATOKA UK. 24

ji wapya wa timu hiyo watakaotumika msimu ujao wa mashindano.

"Hakuna mchezaji tutakayemkosa katika wale tunaowataka, Kocha wetu alishatoa maoni yake kwenye ripoti aliyotuachia na wachezaji ambao amewapendekeza tutawasajili na watakuwepo kwenye kikosi chetu msimu ujao," alisema Ahmed.

Dirisha la usajili lililofunguliwa jana litafungwa Agosti 31 na Shirikisho la soka Tanzania (TFF) limezitaka klabu za Ligi Kuu, Ligi daraja la kwanza na Ligi daraja la pili kukamilisha usajili wa wachezaji wao ndani yakipindi hicho.

## Yanga, CRDB mambo safi

INATOKA UK. 24

alisema Injinia Hersi.

Alisema kupitia makubaliano hayo, Yanga itanufaika katika maeneo tofauti, yakiwemo ya kuhudumia wanachama na mashabiki wao wote kupitia matawi na mawakala wa benki hiyo kote nchini na kupata kadi kwa haraka, pamoja na promosheni mbalimbali za benki hiyo.

"Wale wenye kadi za awali chini ya N-Card watatakiwa kwenda CRDB kuhuisha kadi kwa kulipia katika utaratibu mpya kwa msimu, yaani Julai Mosi mwaka huu hadi Juni 30 mwakani, ambaye si mwanachama wa Yanga, ila ni mteja wa benki hii atatakiwa kufika tawini kuunganisha akaunti ya uanachama na kadi tayari kujisajili na kufanya malipo," alisema Hersi.

Kwa upande wake Ofisa Biashara Mkuu wa benki hiyo Boma Rabala alisema kuanzia Julai 5 mwaka huu benki hiyo itatoa ofa kwa wanachama kuchukua kadi za usajili bure zoezi ambalo litachukua muda wa mwezi mmoja.

"Kwa upande wetu tumeamua kuwapa ofa wanachama kuchukua kadi bure ndani ya mwezi mmoja isipokuwa anatakiwa kulipa ada ya uanachama pekee kwani tutakuwa tupo tayari kuanza zoezi hilo,"alisema Ramala.

Ofisa huyo alisema zoezi hilo litakwenda kusaidia timu ya Yanga kupata shilingi bilioni 20 kwa ajili ya msimu ujao kupitia ada ya wanachama .

"Makubaliano haya yanaenda kuweka alama kubwa katika Sekta ya Michezo Tanzania na kubadili mfumo na mitazamo yote ya kifedha kwa wapenda soka kupitia huduma za kidigitali za benki yetu, tunawushukuru uongozi wa Yanga kutupa nafasi hii ya kuhudumia wanachama wa klabu hiyo pendwa," alisema Ramala.

Michezo

Jumapili Julai 2, 2023

Nipashe



Pulisic akubali kujiunga na Milan

UKURASA 21



Wachezaji wa timu za vijana za Mtibwa Sugar na Azam FC wakiwania mpira kwenye mchezo wa nusu fainali ya ligi ya vijana uliochezwa juzi Uwanja wa Azam Complex, Mtibwa ilishinda mabao 2-1 na kuungana na Geita Gold FC kucheza fainali ya michuano hiyo leo. **PICHA:MTANDAO**

# Yanga, CRDB mambo safi

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga jana imesaini makubaliano na benki ya CRDB yakiwa na lengo la kuongeza ufanisi wa Usajili wa Wanachama na Mashabiki, pamoja na kuwapa suluhishi za kifedha kupitia kadi zao za wanachama zitakazotolewa kwenye matawi ya benki hiyo kuanzia Julai 5.

Akizungumza mara baada ya kutiliana saini ya makubaliano hayo, Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said, alisema kwa sasa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo hawatapata usumbufu wa usajili kama walivyokuwa wakipata kipindi cha nyuma walipokuwa wakitumia kadi za N-Card.

"Baada ya mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji, Usajili wa Wanachama ulikuwa unafanywa matawini mwetu na Kampuni ya N-Card, ambao ulituwezesha kupata takribani wanachama 49,000, hata hivyo tukapata changamoto ya sehemu za kuwasajilia na pili ucheleweshaji wa kadi baada ya usajili.

"Lakini kwa sasa mashabiki na wapenzi wa klabu yetu niwahakikishie changamoto hizo zote na nyinginezo, zinaenda kumalizwa na makubaliano haya na CRDB, wenzetu watatumia matawi yao na Mawakala wao waliotapakaa kote nchini, ndio maana nasema tatizo la usajili na ucheleweshaji kadi limefikia ukomo, tumepata mshirika sahihi ambaye ni CRDB,"

INAENDELEA UK 23

# SIMBA YAANZA MAZUNGUMZO NA KIUNGO AUBIN KOAUME

## ●●● Kuwagharimu shilingi milioni 300, yaachana rasmi na Ismail Sawadogo....

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha la usajili likifunguliwa rasmi jana, Simba ipo kwenye mazungumzo na ipo kwenye hatua nzuri za kukamilisha usajili wa kiungo mshambuliaji wa klabu ya Asec Mimosas ya Ivory Coast, Aubin Kramo Koaume, huku wakitangaza kumuacha rasmi kiungo Ismail Sawadogo.

Jana jioni Simba iliandika kwenye mtandao wake rasmi kufikia makubaliano ya kuachana na mchezaji huyo waliyemsajili wakati wa dirisha dogo msimu uliopita.

Sawadogo licha ya kutegemewa kufanya makubwa ndani ya klabu hiyo, alishindwa kuonyesha makali na kuonekana kuwa mchezaji wa kawaida na hivyo uongozi kuamua kuachana naye.

Simba sasa ipo kwenye mazungumzo na Koaume ya kumsajili kwa ajili ya msimu ujao wa ligi kuu na mashindano ya kimataifa.

Imeelezwa kiungo huyo ataigharimu Simba kiasi cha shilingi milioni 300 na uongozi wa klabu upo kwenye mazungumzo na nchezaji huyo.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema Simba inataka kumsajili mchezaji huyo kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho baada ya kuondoka kwa Sawadogo, Augustine Okra, lakini pia kuwepo uwezekano wa kumuuza Pape Sakho kwenye klabu ya K.V.C. Westerlo ya Ubelgiji.

Klabu hiyo ya Ubelgiji inadaiwa kuwa ipo tayari kulipa dola za Marekani 500,000 (zaidi ya Sh. bilioni moja) ili kumnunua mchezaji huyo raia wa Senegal.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo aliiambia Nipashe jana kuwa tayari wameanza kusajili na muda wowote wataanza kutambulisha wachezaji wao wapya waliomalizana nao.

"Tulisema mashabiki na wanachama watulie mambo mazuri yanakuja, sasa kwa sababu dirisha la usajili limeshafunguliwa tutaanza kuwatangazia wachezaji tuliowasajili, Jumatatu (kesho) tutaanza kuachia jina moja baada ya lingine, tulieni," alisema Ahmed.

Mbali na mchezaji huyo, tayari Simba inadaiwa imeshamalizana na winga wa kushoto raia wa Cameroon anayeichezea Rayon Sport ya Rwanda, Leandre Essomba Onana na kilichobakia ni kumtangaza tu.

Lakini pia wapo kwenye mazungumzo ya mwisho na beki raia wa Cameroon Che Fondoh Malone.

Awali Ahmed alisema Jijini Dar es Salaam kuwa wachezaji wote ambao timu hiyo imewalenga kuwasajili itakamilisha usajili huo na kuwatangaza kuwa wacheza-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >